# Nipashe

Ijumaa Juni 26, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580268

www.ippmedia.com

The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710







## Shambulio mishale dhidi ya walimu lazua taharuki

UKURASA 4

# Ajali ya boti ilivyoua tisa Ziwa Tanganyika

**51** waokolewa. Ni baada ya kupigwa na dhoruba... *Endelea ukurasa 2*



Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zubeir (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kufunguliwa kwa madrasa na kuwatangazia Waislamu kuwa ibada ya Hijja kidunia haitakuwapo isipokuwa kwa waumini waliopo ndani ya Saudi Arabia. **Habari Uk. 3**. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## MWANACHUO ADAIWA KUUA MWENZAKE WAKIGOMBEA MSICHANA

UKURASA 2

## Utata Lissu kugombea urais kupitia CHADEMA



UKURASA 2

### BAA LA CORONA



Watoto na watu wazima wanashauriwa kufuata mwongozo wa kujikarantini na kujitenga kama walikutana na watu wenye ugonjwa au dalili ya corona. WHO

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play   App Store



MICHEZO   YANGA YAPATA 'PIGO' LINGINE UK.24   MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Boti yaua tisa, 51 waokolewa

**NA Pendo Thomas,** KIGOMA

WATU tisa wamefariki dunia na wengine 51 kuolewa, baada ya boti ya MV. Nzaimana kuzama katika Ziwa Tanganyika .

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoa wa Kigoma, Martin Otieno, alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya alfajiri wakati boti hiyo ikiwa safarini kutoka eneo la Sibwesa wilayani Uvinza kuelekea Ikola, mkoani Katavi.

Kamanda Otieno alieleza kuwa taarifa za awali zinaeleza boti hiyo ilikuwa imebeba abiria wapatao 60 wakiwa na mizigo yao midogo midogo na bidhaa zingine.

Kwa mujibu wa Kamanda Otieno, wakiwa wanaendelea na safari boti hiyo ilipigwa na dhoruba kisha kuzama.

"Taarifa tulizonazo hadi sasa hivi kuna watu tisa wameopolewa wakiwa wamekufa, kati yao wanawake saba na wanaume wawili," alisema.

Hata hivyo, Kamanda Otieno alisema asingeweza kueleza kwa undani kuhusiana na tukio hilo kwa kuwa alikuwa njiani kuelekea eneo la tukio kuona uhalisia.

Alisema kuwa baada ya kufika na kushuhudia, atauelezea zaidi undani wa tukio lilivyokuwa .

**MGANGA MKUU WA WILAYA**

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Dk. Ruben Mwakilima, aliieleza Nipashe kuwa walipokea majeruhi watatu wa ajali hiyo kwa ajili ya matibabu katika zahanati ya Sibwesa majira ya asubuhi, huku wengine wakiendelea na ratiba zingine kutokana na kutopata athari zozote.

Dk. Mwakilima alisema hadi kufikia jioni, walikuwa wamepokea miili ya watu sita kutoka eneo la tukio.

# Mwanachuo atuhumiwa kuua mwenzake chuoni

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MWANAFUNZI wa Chuo cha Utumishi Kange, jijini hapa anadaiwa kumuua mwanafunzi mwenzake kwa kumchoma kisu baada ya kumkuta kwenye chumba cha rafiki yake wa kike.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi, Blasius Chatanda, alithibitisha jana kwa njia ya simu kutokea kwa tukio hilo, na kueleza kuwa palitokea ugomvi baina ya wanafunzi wa kiume.

Ugomvi huo ulizuka juzi, baada ya kukutana kwenye chumba cha msichana huyo, huku kila mmoja akiona kuwa ana haki ya kummiliki msichana huyo.

Kwa mujibu wa Kamanda Chatanda, aliyefariki dunia katika tukio hilo ni Hussein Daud, ambaye anadaiwa alichomwa kisu na Waziri Ramadhan.

Alifafanua kuwa Daudi alikutwa ndani ya binti huyo.

"Huyu Hussein Daudi aliuawa kwa kuchomwa kisu na mtu anayedaiwa kuwa ni Waziri Ramadhan kwa sababu ya wivu wa mapenzi," alisema na kuongeza:

"Walikutana kwenye chumba cha binti huyo, ndipo walipoanza kugombana wakidhani kuwa kila mmoja anayo haki ya kumiliki."

"Sasa katika ugomvi huo wakiwa chumbani kwa msichana huyo, Waziri Ramadhan alichukua kisu na kumchoma Daud na kusababisha kifo chake papo hapo."

Aidha, Kamanda Chatanda alisema tukio hilo haliwezi kufananishwa na tukio la fumanizi, na kwamba vijana hao wote wawili wamekatisha ndoto zao.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Chatanda aliwataka wanafunzi kuzingatia masomo kwa kuwa hicho ndicho kilichowapeleka hapo.

Kamanda huyo alisema wanamshikilia binti huyo, huku mtuhumiwa akidaiwa kukimbia.

# Utata Lissu kuwania urais 2020

**Na Mary Geofrey**

NIA ya Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, kuwania urais mwaka huu inaonekana kuwa na utata baada ya uongozi wa chama hicho kubainisha kuwapo vikwazo.

Chama hicho kikuu cha upinzani nchini kwa sasa, kimesema mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki anashindwa kurejea nchini kutoka Ubelgiji kutokana na Jeshi la Polisi kushindwa kumhakikishia usalama wake.

Kimesema bado Lissu ana shaka ya usalama wa maisha yake kwa kuwa tangu Desemba mwaka jana, chama kimekuwa kikiliandikia barua Jeshi la Polisi kuomba ulinzi wa kiongozi huyo atakaporejea nchini, lakini hazijibiwi.

Kutorejea kwa Lissu kipindi hiki cha mchakato wa uchaguzi kunaibua utata wa namna atakavyochukua fomu ya kuwania urais kwa kuwa taratibu za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) zinataka aliyetia nia, kufika kwenye ofisi za tume kuchukua fomu.

Lissu (52), ambaye ni miongoni mwa makada 11 wa CHADEMA, waliojitokeza kutangaza kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu, yuko nje ya nchi kwa takriban miaka mitatu baada ya kushambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana jijini Dodoma Septemba 7, 2017.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema Lissu licha ya kujitosa kuomba ridhaa ya chama kusaka kiti cha urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, bado hajahakikishiwa usalama wake na Jeshi la Polisi pindi atakaporejea nchini.

Mnyika alidai kuwa mara kadhaa uongozi wa CHADEMA umemwandikia barua Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, kuomba ulinzi kwa Lissu wakati ataporudi, lakini hawajajibiwa.

"Ukimya wa Polisi kuhusu usalama wa Lissu umesababisha Makamu Mwenyekuti wa CHADEMA (Lissu), aliyeko ughaibuni kutorejea nchini licha ya kukamilisha matibabu yake," alisema.

Mnyika alidai kuwa IGP Sirro ameshindwa kujibu maombi yao waliyotuma kwa barua mbalimbali ikiwamo ya Desemba 23 mwaka jana.

"Lissu amekamilisha matibabu yake. Licha ya kuandika barua na kukumbusha Januari 7, mwaka huu, bado hutujapatiwa majibu ya ombi letu, kimya chako hakipendezi IGP," Mnyika alimlalamikia kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi.

Mnyika alisema CHADEMA kinaendelea kushirikiana na Lissu kuangalia namna watakavyoshughulikia safari yake ya kurejea nchini, huku akibainisha kuwa taratibu za chama chao hazimnyimi mwanachama aliye nje ya nchi nafasi ya kuwania urais.

"Kutojibiwa na IGP haiwezi kuwa kikwazo, sisi kama chama kwa kushirikiana na Lissu tutalishughulikia hili jambo, kwa kuwa IGP amejitokeza mbele ya habari kuzungumzia ujio wa Lissu, aulizwe aeleze kwanini hajajibu barua ya (Freeman) Mbowe (Mwenyekiti wa CHADEMA) kuhusu Lissu kuhakikishiwa usalama wake," Mnyika alisema.

Jumatatu, IGP Sirro, akizungumza katika mahojiano na ITV, pamoja na mambo mengine, aligusia suala la kushambuliwa kwa Lissu, akisisitiza kuwa wanamsubiri kwa hamu mtaalamu huyo wa sheria baada ya kusikia anatarajiwa kurejea nchini mwaka huu kuwania nafasi ya urais katika uchaguzi ujao.

IGP Sirro alisema Lissu na dereva wake ni watu muhimu katika upelelezi wa Jeshi la Polisi kuhusu tukio la kushambuliwa kwa Lissu na kwamba kamwe jalada la uchunguzi wa suala hilo halitafungwa hata kama Lissu atarejea nchini baada ya miongo miwili.

Hata hivyo, katika mahojiano hayo, IGP hakuzungumzia tuhuma zilizoelekezwa kwake na Mnyika za kutojibu barua za uongozi wa CHADEMA kuhusu kumhakikisha usalama Lissu atakaporejea nchini.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jana, Mnyika pia alilitaka Jeshi la Polisi kutoa ushaidi wa tukio la kuvamiwa na watu wasiyojulikana kwa Mwenyekiti wa Chadema, Mbowe.

Alisema katika tukio la kushambuliwa kwa Mbowe, Jeshi la Polisi limejaribu kuonyesha kama vile hakushambuliwa na kwenda mbali zaidi kwa kudai wanakusudia kumpeleka mahakamani.

"Kama kuna ushahidi wanayoyasema kuhusu tukio la kushambuliwa Mbowe, basi watoe ushahidi na mashahidi. Kuna maneno haya ya kusema alikuwa amelewa, basi madaktari waliompokea waseme," Mnyika alisema.

Katika mahojiano yake na ITV Jumatatu, IGP Sirro alizungumzia madai ya kushambuliwa kwa Mbowe, akibainisha kuwa Jeshi la Polisi lililazimika kutumia nguvu kumhoji dereva wa kiongozi huyo baada ya kuwa amezuiwa kuzungumza chochote kuhusu tukio hilo.

IGP Sirro pia alisema wanakusudia kumfungulia mashtaka mahakamani Mbowe ikiwa upelelezi wao unaoendelea, utabaini alitoa taarifa za uongo kuhusu tukio hilo.



Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**


MRASHI AUCTION MART & BROKERS LIMITED

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA / NOTISI**

**MRASHI AUCTION MART & BROKERS LIMITED** inatoa **NOTISI** ya mdaiwa ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya gazetihili, kwa Mdaiwa afuatae awe amelipa deni lote pamoja na gharama za YADI.

| SN | JINA LA MDAIWA / MDHAMINI | MAHALI | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO DHAMANA |
|---|---|---|---|
| 1. | DICKSON W. URIO | DAR ES SALAAM-ILALA | Gariainaya HICHA YenyenambayausajiliNo.T 722 DBGiliyopoMkoawa Dar essalaam,Manispaaya ILALAyenyejina la DICKSON .W. URIO |

**MASHARTI YA MNADA**
**Dhamanazitauzwamahalizilipo**

1. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alicho shinda mara tu dalali atakapo mtangaza kuwa mshindi (nyundoitakaposhushwa), salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya siku 14 kutokasikuyamnada. Kiasi chaasilimiaishirinitano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha sikukumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
2. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifazanyaraka za umiliki ni za mnunuzi.
3. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa nyumba, gari au kifaa / vifaa alivyo nunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

115789502

**Kwamawasiliano Simu: +255 712 576 523**
**WOTE MNAKARIBISHWA.**

# Mufti Zubeir aruhusu madrasa kuanza

**Na Romana Mallya**

MUFTI Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakary Zubeir, amewatangazia waislamu wote Tanzania kuwa, kutokana na janga la virusi vya corona kupungua nchini, kuanzia sasa madrasa zinaruhusiwa kuendelea.

Sheikh Zubeir aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwa niaba ya Baraza Kuu la Waislam Tanzania na Tanzania Hard Mission.

Katika mkutano huo alizungumzia mambo mawili ambapo ni hilo la kufunguliwa madrasa na kuwatangazia Waislam kuwa ibada ya Hijja kidunia haitakuwapo isipokuwa kwa waumini waliopo ndani ya Saudi Arabia.

Akizungumzia kuhusu madrasa, Sheikh Zubeir alimpongeza Rais John Magufuli kwa namna ambavyo alivyoongoza taifa dhidi ya corona.

"Tunamuombea kwa Mungu ili azidi kumshika mkono katika shughuli za kila siku," alisema.

Alisema shughuli za madrasa zinaruhusiwa kuendelea kama ilivyokuwa awali kwa sharti la kufuata masharti ya kujikinga.

Kuhusu ibada ya Hijja alisema Baraza hilo linaunga mkono uamuzi huo kwa kuwatangazia waislam kuwa hakutakuwa na fursa ya ibada ya Hijja kwa mwaka huu.


## KAPALAMA AUCTION MART
## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na Mkuti Finance Limited tutauza dhamana za wadaiwa Toyota Allion **T 278 DMX,** Scania Tractor **T 736 AXF,** Toyota Land Cruiser Prado **T 462 BMR,** Toyota Hilux **T 780 AAV.**

**Kwa mawasiliano:**
**Kapalama Office 0714 300700/0655 756490.**
**Mkuti Finance Ltd 0715 496544.**

215789602


# NEC yasubiri tangazo la kuvunjwa Bunge

**Na Romana Mallya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imesema inasubiri tangazo kwenye gazeti la serikali la kuvunjwa kwa Bunge ili waweze kuweka tarehe rasmi ya Uchaguzi Mkuu.

Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, aliliambia Nipashe kuwa, mpaka sasa ratiba ya uchaguzi haijatoka kwa sababu hizo za kisheria.

"Ratiba bado haijatoka mpaka utaratibu wa kisheria kujua Bunge limevunjwa lini, hii ni mpaka tangazo litakapotoka kwenye gazeti la serikali kuwa Bunge limevunjwa rasmi lini ndipo sisi tutawatangazia," alisema.

Hivi karibuni, akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha alisema baada ya tangazo hilo tarehe ya kufanyika kwa uchaguzi itatangazwa.

Alisema Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kifungu 37(1) kinaielekeza Tume kufanya uteuzi kwa wagombea nafasi ya kiti cha urais, ubunge na udiwani.

Pia, Mahera alisema, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kifungu cha 46(1), kinasema kuwa tarehe ya uteuzi wa wagombea itatakiwa kutajwa ndani ya siku 60 hadi 90 na kutangaza siku ya uchaguzi.

# Waomba serikali kuongeza vituo vya CTC

**Na Welingtone Masele,** URAMBO

BAADHI ya watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU) wilayani Urambo, wameiomba serikali kuongeza vituo vya kutolea huduma na dawa (CTC) katika vituo vyote vya afya na zahanati ili kuwaondolea changamoto ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hizo.

Wakizungumza katika mkutano uliohudhuriwa na Mkuu wa Mkoa huo, Aggrey Mwanri juzi, walisema wanapata wakati mgumu kutokana na wilaya hiyo kutopanua wigo wa vituo vya wenye VVU ambao wapo zaidi ya 30,000.

Walisema changamoto hiyo inasababisha baadhi yao kushindwa kufika katika vituo vya kutolea huduma hizo kutokana na gharama kubwa za usafiri.

Pia, walisema wenzao wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za usafiri huamua kuacha kutumia dawa za kufubaza virusi hivyo jambo linalosababisha wengi wao kupata madhara ya kiafya.

Mratibu wa Ukimwi, wilayani humo, Dk. Joyce Ongati, alisema wilaya hiyo ina vituo 10 pekee vinavyotoa huduma ya CTC kati ya 31 na kwamba wamekuwa wakifanya utaratibu wa kutoa huduma kwa njia ya mukoba kwa kupita katika maeneo yasiyokuwa na vituo ili kutoa huduma na kuwafikia walengwa kwa urahisi.




RIPOTI MAALUMU

# Shambulio mishale dhidi ya walimu lazua taharuki

## Mmoja auawa, mwingine ajeruhiwa

**Na Idda Mushi,** GAIRO

WALIMU katika Kijiji cha Chihwanga, Kata ya Itaragwe wilayani Gairo mkoani Morogoro, wamejikuta katika taharuki kutokana na mfululizo wa matukio ya mashambulizi dhidi yao kwa kutumia mishale yaliyosababisha kifo cha mmoja wao.

Kijiji hicho kiko umbali wa kilometa 40 kutoka mjini Gairo, na hadi sasa mwalimu mmoja ameuawa kwa kile kilichodaiwa wivu wa mapenzi na mmoja kujeruhiwa kutokana na kile kinachohusishwa na ushahidi alioutoa kwa vyombo vya dola kuhusu tukio la kushambuliwa kwa mwalimu mwenzake.

Kutokana na matukio ya kushambuliwa kwa walimu, baadhi ya wawezeshaji hao wa taaluma kwa wanafunzi wameomba kuhamishwa kituo cha kazi, lakini hadi sasa hawajafanikiwa.

Matukio hayo yalitokea mwishoni mwa Februari mwaka huu kwa mwalimu wa kwanza kuchomwa mshale na Juni 20 mwaka huu, mwalimu mwingine alipochomwa mshale katika eneo la uwanja wa shule ya msingi, karibu na eneo alikouawa mwalimu wa kwanza na sasa majeruhi huyo amelazwa Kituo cha Afya Gairo.

Nipashe ilizuru katika kijiji hicho na kumtembelea kituo cha afya Mwalimu Hosea Kikoye wa Shule ya Sekondari Iyogwe, ambaye ana majeraha kwenye mkono wa kushoto.

Akisimulia tukio hilo, mwalimu huyo alisema lilitokea Juni 20 mwaka huu, majira ya saa tatu usiku, kwenye uwanja wa mpira wa shule, jirani kidogo na nyumba anayoishi ambazo ni za shule, wakati akitoka kwenye shughuli zake (ana duka) jirani na eneo hilo.

"Nilivamiwa na watu ambao siwafahamu, nilishangaa tu nikiwa njiani namulikwa na mwanga baadaye ukazimwa. Nilishtuka nikapigwa mshale wa mkono.

"Ninafikiri lengo lengo lao lilikuwa wanipige kifuani, Mungu alinisaidia, nilipiga kelele walijitokeza baadhi ya walimu na wanakijiji wema wakanipeleka kupata huduma ya kwanza," Mwalimu Kikoye alisimulia.

Mwalimu huyo alilihusisha tukio la kushambuliwa kwake na ushahidi alioutoa polisi kuhusu mauaji ya mwalimu mwenzake, Madaraka Mwanilwa, aliyeuawa kwa kuvamiwa na watu wasiojulikana na kuchomwa mshale shingoni Februari 24 mwaka huu kwenye uwanja huo huo.

"Hii ni mara ya pili, ninadhani lengo lao kubwa ni kufuta ushahidi, baada ya awali kumsaidia mwalimu mwenzangu aliyepigwa mkuki na mimi kumsaidia, lakini baadaye akafariki, niliitwa polisi kuhojiwa maswali mbalimbali kuhusu kifo chake na nilieleza kila kitu nilichoelezwa na marehemu kabla hajafariki dunia," alisema.



Baadhi ya Walimu wa Shule ya Sekondari ya Iyogwe, katika kijiji cha Makuyu, wilayani Gairo, mkoa wa Morogoro, wakizungumza na Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) wa wilaya hiyo, (wa pili kulia), nje ya Kituo cha Afya Gairo, jana. **Picha ndogo chini:** Mwalimu Hosea Charles, aliyejeruhiwa kwa mkuki akiwa wodini. **PICHA: IDDA MUSHI**.

Aliendelea kusimulia kuwa kufuatia tukio la kuuawa kwa mwalimu huyo, baadhi ya watu walikamatwa na kufikishwa mahakamani na baadaye kesi ilihamishiwa mjini Morogoro.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Gairo, Dk. Bonithe Calist, aliyempokea majeruhi huyo, akizungumza na Nipashe, alisema majeruhi huyo alifikishwa hospitali akiwa na maumivu makali na mshtuko.

Kuhusu mshale aliochomwa kuwa na sumu au la, Dk. Calist alisema kitaalamu siyo rahisi sana kugundua kwa haraka, lakini jitihada zimefanyika ili sumu isisambae mwilini.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Iyogwe, Maria Mdoe, alithibitisha kutokea kwa matukio hayo na kusema kuwa ni mfululizo wa matukio yenye kuzua taharuki kwa watumishi wa kada hiyo.

Alisema matukio hayo yanashusha morali ya kazi kwa shule ambayo imeshika nafasi ya pili kiwilaya kwenye matokeo ya kidato cha nne mwaka jana, kwa kuwa walimu sasa wanaishi kwa hofu ya maisha yao.

"Tukio hili linatukumbusha la Mwalimu Madaraka Mwanilwa, hatujui ni vuguvugu la kitu gani lilikuwa linaendelea bila sisi kufahamu hadi Mwalimu mwingine Hosea Charles alipopigwa mshale," alisema.



Kwa mujibu wa Mwalimu huyo, Mwanilwa aliwahi kuomba kuhamishwa kituo tangu Oktoba mwaka jana baada ya kuwa amefundisha kwenye shule hiyo kwa zaidi ya miaka 10, lakini hadi sasa, taratibu za ngazi za juu hazijakamilika.

"Ninaiomba serikali iliangalie suala hili, huenda itaondoa matatizo kama haya yaliyojitokeza ya kifo na taharuki kwa walimu. Kwa mazingira ya namna hii ambayo walimu wanawindwa kama swala, hatuwezi kuvumilia ndiyo maana tunaomba serikali itusaidie,"alisema.

Kwa mujibu wa mkuu wa shule huyo, mwalimu aliyeuawa na kuzikwa mkoani Iringa, alichukiwa kijijini kwa vile ni msomi na mchapakazi, na hata akijichanganya na wanakijiji alikuwa anatengwa kwa madai kuwa ana majivuno.

"Tunadhani ilikuwa ni sababu ya wao kumwinda na kumuua, na huyu wa pili aliyejeruhiwa inaonekana walisikitika kwa kuona kwanini walimu hawa walisaidiana, na kwanini walipohojiwa polisi walitaja baadhi ya wanakijiji.

"Ni kweli walimu wengine karibu wanne wanatajwatajwa kulipiziwa kisasi kwa sababu kama hizo, walimu wote waliopo hapa siyo wazawa wa Mkoa wa Morogoro, lakini jamii inapaswa kuelimishwa kuwa kila Mtanzania ana sifa ya kuishi popote bila kuvunja sheria.

"Kutokana na hizi taarifa zinazoendelea zinazofanywa walimu wasijiamini, hata kitaaluma shule haitakaa vizuri sana, ingawa mwaka jana tulikuwa wa pili kiwilaya.

"Walimu sasa wamevunjika moyo na kukata tamaa kabisa kutokana na matukio haya kuwa ya mfululizo na ya aina ileile," mkuu wa shule huyo alilalamika.

Mwalimu huyo anasema shule ilikuwa na walimu 24, lakini wengi walihama kutokana na matatizo mbalimbali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, akifafanua: "Alichomwa mshale na mtu asiyejulikana, akakimbilia kwa walimu wenzake na wakamsaidia kumpeleka Zahanati ya Iyogwe na baadaye kuhamishiwa Kituo cha Afya Gairo kwa matibabu zaidi baada ya kuonekana anavuja damu nyingi.

"Sasa hali yake inaendelea vizuri na sisi tunaendelea kuchunguza tukio hili na waliohusika."

Kamanda Mutafungwa pia alithibitisha kuuawa kwa mwalimu katika shambulio la Februari, wahusika wakitumia mishale na chanzo kikidaiwa kuwa wivu wa kimapenzi.

Alibainisha kuwa watuhumiwa wawili wa tukio hilo la kwanza walifikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani humo wakikabiliwa na kesi namba 34/2020.

Mmoja wa wakazi wa Gairo, Jeremiah Mwegoha, alisema alishuhudia baadhi ya wanakijiji wakikamatwa na Jeshi la Polisi baada ya kutokea kwa tukio la kwanza.

Aliomba serikali na vyombo vya usalama kufuatilia kwa kina suala hilo, ili kuondoa taharuki hiyo na kurejesha uhusiano mwema baina ya pande zote.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kijiji hicho, Andrea Majosti, alisema mara kwa mara wanaelimisha jamii kuhusu mambo mbalimbali na hakuna ugomvi baina ya kijiji na shule hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Siriel Mchembe, akiiongoza kamati yake ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya akiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, Agness Mkandya, na maofisa wengine katika halmashauri hiyo, walizuru kijijini huko Jumanne na kuzungumza na wananchi na walimu katika mikutano tofauti.

Eneo hilo la Iyogwe limekuwa likidaiwa kuwa na dosari ya kuwekwa masharti magumu kwa watu wageni wanaoingia huko kwa lengo la kuweka makazi.

Kwa mujibu wa wakazi wa eneo hilo waliozungumza na Nipashe, baadhi ya masharti kwa wageni kaya kutakiwa kuchota maji ndoo moja pekee kwa siku kwa matumizi mbalimbali, kuzuiwa kutwanga chochote kuanzia saa 12 jioni ili kukidhi mila na desturi zilizoelezwa ni za Kikaguru ambao ndiyo wenyeji wa eneo hilo.

# Watatu zaidi wajitokeza kuwania urais Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANACHAMA watatu wa CCM wameongeza idadi ya watu waliochukua fomu ya kuonyesha nia ya kugombea urais wa Zanzibar kufikia 29 visiwani Zanzibar.

Pereira Ame Silima, ambaye ni Katibu wa Idara ya Oganaizesheni ya Kamati Kuu ya chama hicho, ndiye aliyeanza kufungua mlango saa 3:10 asubuhi kuchukua fomu ya kuwania nafasi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Pereira alisema, kilichomsukuma kushiriki ni kuhakikisha kuwa anaitumia haki yake ya kidemokrasia ambayo ipo kwenye Katiba ya CCM.

Perera alisema amechoka kuwa msindikizaji wa kwenda kupiga kura kumchagua Rais.

"Nimechoka kuwa napiga kura tu kuchagua nami nimeamua kwa hili sasa nisimame mwenyewe ili niweze nami kutoa fursa ya wanachama kuamua kuhusu mimi," alisema.

Alisema sababu kubwa iliyomfaya achukue fomu ni kuwa na uchungu na Zanzibar licha ya kwamba viongozi waliopita wamefanya mambo mazuri ya kimaendeleo.

Alisema, ameona ana mchango mkubwa wa kusimamia uendeshaji wa serikali, na vitu vikubwa ambavyo vimemshwawishi ni kuwa nchi inahitaji maendeleo makubwa ya kiuchumi.

"Tunahitaji maendeleo ya kiuchumi kwani bado kipato cha wananchi na serikali ni kidogo, jambo langu la kwanza kufanya nitahakikisha kwamba tunafanya miundombinu ya kutosha ili uchumi wetu ukue haraka," alisema.

Eneo lingine alisema ni la jamii yenye umoja na mtu yeyote kutomuogopa mwezake wala kumbagua huku akiweka kipaumbele katika sekta za elimu, afya.

Pia, atahakikisha anatafuta njia nzuri ya kumaliza tatizo la udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto vinavyoendelea Zanzibar kutokana na hali kutoridhisha.

Mwanachama mwingine aliyechukua ni Iddi Hamad Iddi, aliyefika ofisi hizo saa 4:30 asubuhi.

Akizungumza na waandishi wa habari, alimpongeza Makamu Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wake Dk. John Magufuli kwa kuiletea heshima kubwa Tanzania ikiwamo kusimamia suala la amani na utulivu na kuwalea vizuri wanachama wao kwa kuwapa demokrasia ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema amejitathmini na kuona uwezo anao wa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Saa 5:00 asubuhi, Shaame Ame Silima, alichukua fomu na kutoa vipaumbele vyake ikiwamo kuyaendeleza aliyoyaacha Dk. Shein kwa kuboresha uchumi hasa katika sekta ya bahari ambayo itasaidia kukuza ajira kwa vijana.

Idadi ya wagombea wanaorejesha fomu pia imeongezeka na kufikia 12. Jana waliorejesha fomu ni Meja Jenerali mstaafu Balozi Issa Suleiman, Mohammed Jaffar Jumanne, Mbwana Yahya, Omar Sheha, Dk. Khalid Salum Muhammed na Rashid Ali Juma.

Baada ya kurejesha fomu hiyo, Rashid Ali Juma ambaye ni mwakilishi wa Jimbo la Amani, alisema anashukuru kukamilisha urejeshaji wa fomu hiyo na kutaja changamoto kuwa ilikuwa kuwapata wadhamini 250.

# EWURA kuvifutia leseni vituo vitano vya mafuta

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetangaza kusudio lake la kuvifutia leseni vituo vitano vya mafuta, vikubwa vikiwa viwili.

Vilevile, vipo vilivyopewa onyo na kimoja kikipewa adhabu ya kulipa faini ya Sh. milioni sita kutokana na kitendo chake cha kuuza mafuta juu ya bei elekezi na kutotoa risiti kwa wateja.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, alisema mamlaka hiyo imefikia uamuzi huo baada ya kutoa muda wa saa 48 za kujitetea kwa vituo hivyo ambapo baadhi vilifanya hivyo na vingine havikutoa maelezo yoyote.

Alivitaja vituo ambavyo vipo kwenye kusudio la kufutiwa leseni ni mteja wa jumla aliyeko Kigamboni jijini Dar es Salaam ambaye ni Mansoor Industry.

Vingine ni kituo cha mafuta cha BO5 Ways Petrol cha Bagamoyo kinachouza kwa rejareja, Mexon Energy Ltd cha Makambako, Mexon Energy Ltd cha Njombe na Olimpic.

Kaguo alitaja vingine ambavyo vimepewa onyo ni Oryx, Star Oil Tanzania Ltd ambaye amechunguzwa na amejitetea, lakini bado wanaendelea kumchunguza na asipoangalia naye atafutiwa leseni.

"Vingine ni Come Oil ambaye alijitetea kuwa hakuwa na mafuta kwa sababu yalishikiliwa, hivyo amesamehewa.

"Kituo kingine ni Mtweve Oil cha Chunya ambacho kilikutwa na kosa mara mbili la kuuza mafuta bei ya juu ya kikomo badala ya Sh. 1,637 walikuwa wakiuza Sh. 1,985, hivyo watatakiwa kulipa faini Sh. milioni sita na kosa jingine ni la kutotoa risiti," alisema.

Hata hivyo, alisema upo utaratibu wa kukata rufani, lakini wanaamini hawatashinda.

Kaguo alisema bodi ya EWURA inakusudia kufanya marekebisho ya leseni za uuzaji wa mafuta na kwamba kabla ya mtu kupatiwa atatakiwa aonyeshe ana vituo vingapi ili kuondoa tatizo la mafuta hasa kwa wateja wa rejareja.

Pia, alikiri kuwapo kwa dalili za baadhi ya watu kuficha mafuta ili kushinikiza bei ipande.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
President's Office – State House
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

**TENDER NO. TZ-TASAF-181607-GO-RFB TO SUPPLY THERMAL SCANNERS**

**Invitation for Tenders**

**Date: 26th June, 2020**

1. This Invitation for Tenders follows the General Procurement Notice for this Project which appeared in UN Development Business Issue no. WB-P475857-02/20 dated 4th February, 2020.

2. The Government of the united republic of Tanzania has received financing from the World Bank toward the cost of the Productive Social Safety Net II. This project will be jointly financed by the Agency for International Development, Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria, International Fund for Agriculture Development, The government of NORWAY and OPEC. The Tanzania Social Action Fund the implementing agency for this Project intends to apply part of the proceeds toward payments for procurement of Thermal Scanners.

3. The The Tanzania Social Action Fund now invites sealed tenders from eligible Suppliers of Thermal Scanners.

4. Tendering will be conducted through the National Competitive tendering procedures specified in the Public Procurement Regulations, 2013 – Government Notice No. 446 as amended in 2016, and is open to all Tenderers as defined in the Regulations.

5. Interested eligible Tenders may inspect the Tendering Documents in the TASAF Website at: www.tasaf.go.tz or obtain further information through the address indicated below.

6. A complete set of Tendering Document(s) in English is available and can be downloaded from the TASAF Website at: www.tasaf.go.tz by interested Tenderers. Amendments and clarifications to the Tendering Documents if applicable will also be posted at the same Website.

7. All tenders must be accompanied by a Tender Securing Declaration in the format provided in the Tendering Documents.

8. All tenders must be addressed as indicated below and submitted via e-mail at or before 10:00 hours East African time on 10th July, 2020

   Electronic Tendering will not be permitted except e-mail submission as detailed in ITB BDS 21.2 in view of COVID-19. Late Tenders will be rejected.

   In view of COVID-19, the public opening will be conducted immediately after the deadline time for submission through live streamed and recorded and the video recorded will be posted for viewing through the TASAF's website: www.tasaf.go.tz. Online tender opening meeting details are indicated in ITB BDS 25.1.

9. Late Tenders, Portion of Tenders, Electronic Tenders, Tenders not received, Tenders not opened and not read out in public at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**Board of Trustee of PSSSF Building,**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**P. O. Box 2719,**
**Dodoma, Tanzania**

215790302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Rushwa isiwe sifa kuu ya kuchaguliwa mwaka huu

**PILIKAPILIKA** za uchaguzi mkuu zimeanza kwa vyama mbalimbali vya siasa kutoa ratiba zao za ndani kuanzia nafasi za urais, ubunge, udiwani na vikao vya kimaamuzi katika kura ya maoni na kuchuja wanaostahili kupeperusha bendera ya chama husika.

Kwa ujumla, kabla ya kufungwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baadhi ya waliokuwa wabunge walijikuta matumbo joto kutokana na baadhi ya watu kuanza kujipitisha huku na kule kuyanyemelea majimbo yao, kiasi cha baadhi ya vyama hususan Chama Cha Mapunduzi (CCM) kutoa onyo kuwa muda wa kufanya hivyo bado.

Rais alivunja Bunge Julai 16, mwaka huu, na kilichosubiriwa ni kutangazwa katika gazeti la serikali ili Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) itoe ratiba ya mchakato wa jumla na kupuliza kipenga kwa vyama kushindania nafasi husika.

Kwa sasa baadhi ya vyama vimeruhusu watu kuchukua fomu za urais na kutia nia katika ngazi nyinginezo, huku kwenye majimbo na kata kukiwa na ongezeko la wanaoonyesha kutaka nafasi hizo huku waliokuwapo wakizitetea.

Tayari Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeshakamata na kuwahoji watu kadhaa ambao kwa namna moja au nyingine walionekana kuanza kampeni ikiwamo kutoa rushwa.

Tofauti na miaka mingine ambayo rushwa ilikuwa ndiyo sifa ya kwanza kwa wenye nia ya kugombea na kama huna fedha huwezi kuwa kiongozi, kwa sasa TAKUKURU imeonyesha makucha yake hadharani na kufanya kwa vitengo kuonyesha kuwa rushwa haikubaliki na haitakiwi katika uchaguzi mkuu wa Oktoba.

Hali hiyo imewarudisha nyuma waliokuwa wamejipanga kutumia fedha chafu kwa ajili ya kununua uongozi, na sasa kila anayeona ana sifa za kuongoza anaweza kuwania nafasi yoyote na kuipata bila kutumia nguvu ya fedha kwa ajili ya kuwashawishi wapigakura.

Jambo hili linaungwa mkono na kupongezwa kwa kuwa sasa tunakwenda kupata viongozi ambao wamekubalika kwa sera na dhamira zao za kuongoza wananchi kwa lengo la kuleta maendeleo na si kwa nguvu ya fedha.

Kwa msingi huo, wagombea wanapaswa kuwa makini sana na kuhakikisha hawajihusishi kwa namna yoyote na vitendo vya rushwa, bali kunadi sera zao, mipango na mikakati kushaishi wapigakura kuwapa nafasi.

Katika hili, tunaisihi TAKUKURU kuendelea kufanyakazi kwa ujasiri, weledi mkubwa na kusiwe na uonevu au kutaka kukomoa yeyote, kwa kuwa tunajua kipindi kama hiki kuna kuchafuana, kuchongeana na kuumizana kisiasa.

Wapo ambao wanaweza kutengeneza matukio ya kutaka kuwaharibia wengine kwa kupeleka taarifa za uongo, lakini tunaamini kwa umahiri na weledi wa taasisi hiyo, hakuna atakayeonewa bali kila mtu kupata stahiki yake kwa kadri ya matendo yake.

Watanzania wanataka viongozi watakaowatumikia vyema, wenye nia ya dhati ya kuwaongoza na kutatua changamoto zilizopo katika maeneo yao, na wakitokana na rushwa maana yake watataka kurudisha fedha zao baada ya kupata nafasi husika.


Lakini wananchi wanapaswa kutambua kuwa kupokea rushwa ni kosa kisheria, wasijenge mazingira ya kupata fedha au takrima kutoka kwa wagombea. Pia, uchaguzi wa rushwa unaweza kuwanyima haki wagombea kutoka katika makundi yenye uhitaji kama wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambao hawana uwezo wa kuwa na fedha za kutoa rushwa.

Tunajua ni vigumu sana wagombea kutoa taarifa za wanaoomba rushwa kuwa kuwa wakifanya hivyo huenda wakakosa kura, lakini ndani ya vyama kumekuwa na malalamiko ya rushwa ambayo yanawaumiza wagombea, lakini hawana pa kusemea na ndiyo maana wengine wakishapata uongozi huwa hawarudi nyuma bali wanatumia muda huo kupooza machungu.

Hatutarajii kuona wagombea wakiishia mikononi mwa TAKUKURU kwa makosa ya kutoa rushwa, bali wajinadi kwa sera na umahiri wao iwapo wapewe ridhaa ya uwakilishi katika nafasi hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kaya hewa zibanwe zaidi kulinda fedha za TASAF

**KATIKA** kipindi cha pili cha awamu ya tatu, mwaka 2020 hadi 2023, jumla ya Sh. trilioni 203 zitatumika, ambapo awamu hiyo utekelezaji utafanyika, kwenye halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na wilaya zote 11 za Zanzibar.

Shilingi trilioni 1.22 katika kiasi hicho cha fedha kilichotengwa, ni sawa na asilimia 60 zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye vijiji na mitaa 16, 596 vya Tanzania Bara na Shehia 388, Zanzibar.

Lengo kuu serikalini ni kuendelea kuboresha maisha ya wananchi wanyonge kwa kutekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Hiyo ni kwa mujibu wa mawasilisho ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alipowasilisha bungeni mapendekezo ya serikali kuhusu makadario ya mapato na matumizi kwa mwaka huu wa fedha.

Dk. Mpango anasema, kipaumbele kipo na kitatolewa kwa watu wenye nguvu wanaotoka kwenye kaya maskini, ambayo ajira milioni 1.2 zitazalishwa na kuwapatia walengwa ujuzi na pamoja na stadi za kazi.

Kimsingi, TASAF inatajwa kuchangia kubadili kwa kiwango kikubwa maisha ya wanufaika na kuwajengea uwezo wa kuanzisha vitega uchumi na kuwafanya wasiwe wategemezi badala yake wanajitegemea kiuchumi.

Lengo kuu ni kupunguza tatizo la umaskini nchini, huku walengwa wakuu wakiwa wananchi wanaotoka katika kaya zisizojiweza na zinazotazamwa kuishi katika umaskini uliotukuka.

Lakini pamoja na juhudi hizo za serikali za kuboresha maisha ya wananchi wanyonge, kumekuwapo changamoto kadhaa, ambazo kwa namna moja au nyingine zinatia doa juhudi hizo.

Baadhi ya changamoto hizo, ni kuwapo kaya maskini na hewa, ambazo zimekuwa zikifaidika na fedha hizo na kusababisha walengwa kukwama. Hivyo, kuna haja ya kuongeza umakini kuzidhibiti kaya hizo.

Matarajio ya kuanzishwa kwa mpango huo, ni kuwapata walengwa halali wanaonufaika, ili kutimiza lengo la Benki ya Dunia na serikali kwa ujumla, ambayo ni kuziinua kaya maskini nchini.

Kwa ujumla ni kwamba mpango wa TASAF wa kunusuru kaya maskini nchini umeonyesha mafanikio makubwa, lakini unaharibiwa na kasoro zinazotokana na baadhi ya watendaji wa halmashauri wanaohusika kukosa uwazi na uadilifu.

Tatizo hili lipo katika uwajibikaji, hali iliyosababisha kufanyika tena uhakiki wa TASAF kwa mwaka 2016 na hata wakabaini jumla ya kaya 55,692 zilizokuwa zinanufaika na mpango, bila ya kuwa na sifa stahiki.

Hiyo ni kwa mujibu wa Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa mwaka 2016/2017, iliyowahi kutolewa na mwenyekiti wake, Jasson Rweikiza.

Inawezekana watumishi au wajanja wachache kutoka kwenye kaya hizo, wakafanya njama na watumishi hao, ili waingizwe katika orodha ya wasiojiweza kwa lengo la kuchukua fedha wagawane.

Lakini, kwa sasa ujanja huo umeshabainika, hatua iliyo nayo serikali sasa ni kuhakikisha hazitokei kaya hewa tena na badala yake, Sh. trilioni 203 zilitengwa zinufaishe walengwa tu.

Hilo likifanyika, matarajio ya mpango huo yatakuwa yametimia, ambayo ni kuona wanufaika halali ndiyo wanafikiwa, kwani vinginevyo, kaya maskini zitaendelea kukwamishwa na wajanja wachache.

Ikumbukwe kwamba, tangu mwaka 2000, mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia mradi wa TASAF, ulianzishwa rasmi nchini, kwa udhamini wa Benki ya Dunia (WB), lengo ni kupunguza tatizo la umaskini kitaifa.

Mara zote, walengwa wakuu wa mpango hui ni wananchi kutoka kaya zisizojiweza, zinazoishi katika umaskini. Matarajio yao yanatiwa doa na wale wasio waaminifu.

Hivyo, umefika wakati kila upande kuwa makini kuhakikisha kwamba kilichokusudiwa kwa ajili ya mpango huo, kinatumia hasa kwa kubana mianya yote inayowezesha wachache kujinufaisha.

Kwa kuwa serikali imeshatambua mchezo huo na kutoa onyo, ni wazi wenye masikio wamesikia ni matarajio kwamba waliokuwa na wazo la kuendelea kuandaa kaya hewa watakuwa wameacha mpango huo.

# Uchunguzi mume anayedaiwa kuua mkewe waendelea

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoa wa Kinondoni, limesema uchunguzi wa tukio la Erick Bubelwa, anayedaiwa kumuua mke wake, Mercy Mkambala, kwa kumshambulia na kitu cha ncha kali bado unaendelea.

Kamanda wa Polisi wa mkoa wa Kinondoni, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Edward Bukombe, aliliambia Nipashe juzi kuwa uchunguzi wa tukio hilo unaendelea.

"Uchunguzi bado unaendelea kama unavyojua mauaji hayana dhamana na uchunguzi wake huchukua muda mrefu bado hatujamfikisha mahakamani, tunaendelea kuchunguza," alisema.

Tukio hilo lilitokea Juni 16, maeneo ya Kimara Stop Over baada ya mume kudaiwa kumshambulia mke wake kwa kitu cha ncha kali eneo la paji la uso na kumsababishia kifo chake.

Akithibitisha tukio hilo, Kamanda Bukombe aliliambia Nipashe, wanamshikilia mume wa marehemu ambaye anadaiwa kuwa chanzo cha kifo hicho.

Mama mdogo wa marehemu, Aglipina Dominic, alisema mama wa marehemu alimpigia simu kumjulisha kuwa, amepokea taarifa kuwa Mercy kapigwa na shoti ya umeme chumbani kwao.

Lakini, alisema baada ya kufika eneo la tukio walikuta mlango umefungwa na askari walikuwa wameshafika na baadaye jioni ulipofunguliwa, walibaini siyo kweli kama walivyosimulia kuwa mtoto wao amepigwa shoti.



Mkuu wa Kitengo cha Biashara cha Halopesa, Magesa Wandwi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa HaloPesa App, itakayowawezesha wateja wao, kufanya miamala mbalimbali kwa urahisi zaidi. Kushoto ni Ofisa Bidhaa na Masoko, Roxona Kadio. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yataka msamaha wa madeni kwa nchi maskini

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuziomba taasisi za fedha za kimataifa pamoja na nchi za Jumuiya ya Madola kufikiria kufuta kabisa madeni yaliyokopeshwa kwa nchi zinazoendelea, ili fedha hizo ziweze kutumika kupambana na athari zilizotokana na Covid-19.

Ombi hilo limetolewa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamamba John Kabudi, alipokuwa akimwakilisha Rais John Magufuli, katika mkutano wa Marais, Mawaziri Wakuu pamoja na Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi na Serikali za Jumuiya ya Madola uliofanyika kwa njia ya mtandao juzi jijini Dar es Salaam.

Prof. Kabudi alisema Tanzania imesisitiza tena umuhimu wa mashirika ya fedha ya kimataifa na nchi za Jumuiya ya Madola zilizoikopesha mbali na kutoa msamaha wa madeni kufikiria kufuta kabisa madeni hayo ili kuziwezesha nchi zinazoendelea kuwa na fedha za kuboresha mifumo ya afya, pamoja na kupambana na athari zilizotokana na janga la Covid-19.

Katika mkutano huo, Tanzania ilisisitiza umuhimu wa kuendeleza ushirikiano kati ya nchi za Jumuiya ya Madola na nchi zinazoendelea ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na umoja na mshikamano katika kupambana na janga la Covid-19.

"Mkutano huu umekuwa ni muhimu sana katika Jumuiya yetu ya Madola na tumesisitiza kuwa kuna umuhimu wa kushirikiana na kuwa na misaada na mipango madhubuti ya mashirika ya kimataifa kuzisaidia nchi zinazoendelea katika jitihada zake za kuboresha na kujenga viwanda vyake hasa vya kutengeneza dawa na vifaa tiba ili inapotokea majanga kama haya ya Covid-19 ziweze kuwa na dawa na vifaa tiba kwa wananchi wake," alisema Prof. Kabudi.

Aliongeza kuwa, nchi nyingi baada ya janga la Covid-19 zilizuia utoaji wa dawa na vifaa tiba kwenda nje ya nchi kwa sababu dawa hizo walizihitaji kwa ajili ya matumizi yao wenyewe ndani ya nchi, na ndiyo maana nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) imeiomba India kwa upendeleo kuipatia dawa na vifaa tiba vya kukabiliana na janga la corona.

Aidha, alisema mkutano ulijadili pia umuhimu wa teknolojia katika kupambana na Covid-19 na kuboresha mifumo ya afya, na kwamba wakati umefika sasa teknolojia hiyo mahali popote ilipo ndani ya Jumuiya ya Madola iweze kutolewa kwa nchi zote kwa gharama nafuu ili kuziwezesha nchi mbalimbali kutumia mifumo mipya ya kiteknolojia katika mifumo yake ya afya na kuziwezesha pia kupambana na Covid-19.

"Ni vizuri tuwe na mipango madhubuti na mikakati ya kupambana na aina hii ya majanga, ambayo yanaweza kujitokeza siku za usoni na kufanya hivyo ni kuanza kujiandaa sasa kwa kuimaraisha huduma za afya katika nchi zetu," alisema Prof. Kabudi.

Waziri Kabudi aliongeza kuwa Tanzania imeanza jitihada hizo kwa kujenga hospitali nyingi za wilaya, mikoa pamoja na vituo mbalimbali vya afya na zahanati.

Mkutano ulijadili, masuala mbalimbali ikiwamo Covid-19, biashara, uchumi, viwanda, uwekezaji pamoja na mabadiliko ya tabia nchi.

Aprili, 2020 Rais Magufuli aliiomba Benki ya Dunia pamoja na mashirika ya fedha ya kimataifa kuzisamehe madeni nchi zinazoendelea ili nchi hizo ziweze kutumia fedha hizo katika mapambano dhidi ya Covid-19.

# Lukuvi abana maofisa ardhi utoaji wa hati

**Na Munir Shemweta,**
ARUSHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amewataka maofisa ardhi nchini kuhakikisha wanawafuatilia wamiliki wa ardhi ambao hati zao zimekamilika, lakini hawataki kuzichukua ili wazichukue katika kipindi cha siku 90.

Lukuvi alitoa agizo hilo jana jijini Arusha alipozindua ofisi ya ardhi ya mkoa huo ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kuzindua ofisi za ardhi katika mikoa mbalimbali nchini.

Waziri huyo ambaye tayari amezindua ofisi za ardhi kwenye mikoa ya Tanga na Manyara, alisema kuwa hivi karibuni Bunge lilipitisha sheria inayotaka mmiliki wa ardhi aliyepimiwa eneo lake, kuchukua hati katika kipindi cha siku 90 na asipofanya hivyo, utaratibu wa kumkata kodi ya pango la ardhi utafanyika.

Kwa mujibu wa waziri huyo, kumekuwa na tabia ya baadhi ya wamiliki wa ardhi kutojitokeza kuchukua hati za viwanja vyao kwa lengo la kukwepa kulipa kodi ya pango la ardhi, jambo linalolielezea kuwa linamnyima fursa mbalimbali mmiliki sambamba na kuikosesha serikali mapato yatokanayo na kodi ya ardhi.

Alitolea mfano wa Mkoa wa Arusha kuwa, pamoja na kuwa na jumla ya viwanja 78,405 vilivyopimwa na hati zake kusajiliwa, ni hati 29,000 pekee zilizochukuliwa na wamiliki wake na hivyo kuwa na hati 49,405 ambazo hazijachukuliwa na kuikosesha serikali mapato ya ardhi.

"Ardhi ndiyo ulinzi wa rasilimali na inachangia kodi ya serikali. Kwa hiyo, wale wote wasiochukua hati, wajitokeze katika kipindi cha siku 90, tunataka idadi ya viwanja vilivyopimwa na kuwekewa mawe ifanane na hati zilizopo na wote waliopimiwa wakachukue, baada ya hapo kama hujachukua hati utaletewa 'invoice' ya malipo," alionya.

Akizungumzia uanzishwaji ofisi za ardhi za mikoa, Lukuvi ambaye alitoa hati 201 kwa wamiliki wa ardhi mkoani Arusha, alisema ofisi hizo zimeanzishwa ili kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi.

Alibainisha kuwa kwa sasa wananchi watapata huduma zote za ardhi kwenye mikoa yao kama walivyokuwa wakipata makao makuu ya wizara na ofsi za ardhi za kanda.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Iddy Kimanti, alipongeza wizara hiyo na Rais John Magufuli kwa uamuzi wa kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi kwa kuanzisha ofisi za ardhi za mikoa na kubainisha kuwa ofisi yake itatoa ushirikiano na kusaidia masuala mbalimbali ya ofisi ya ardhi kwenye mkoa wake, ili kufanikisha azma ya serikali.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, pia alimshukuru Rais Magufuli kwa kuwezesha utekelezaji jukumu la kusogeza huduma za sekta ya ardhi karibu na wananchi kwa uanzishaji ofisi za ardhi za mikoa.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Arusha, Leo Komba, alibainisha kuwa, tangu kuanzishwa kwa ofisi yake Machi mwaka huu, tayari hati 210 zimeandaliwa na 101 kutolewa kwa wamiliki wake, huku miamala 282 ikiwa imefanyika na michoro 19 yenye viwanja 4,196 kuandaliwa sambamba na ramani 29 zenye viwanja 133 kuidhinishwa.

# Mil. 780/- kujenga kliniki ya huduma za methadone

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wanaendelea kuboresha huduma za afya nchini ambapo Sh. milioni 780 zimetolewa kwa ajili ya kujenga kliniki ya huduma za methadone kwa waathirika wa dawa za kulevya mkoani Tanga.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, wakati wa uzinduzi wa kituo cha muda cha kutoa tiba ya methadone kwa warahibu wa dawa za kulevya kilichopo katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga - Bombo.

"Kwa kushirikiana na wadau wetu wa maendeleo Mfuko wa Dunia (Global Fund) na Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za kulevya tumepata zaidi ya Sh. milioni 780 na tumezileta kwa ajili ya kujenga jengo la kutolea huduma ya methadone," alisema Waziri Ummy.

Aliupongeza uongozi wa mkoa wa Tanga kwa ubunifu walioufanya kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wakiwamo PEPFAR na Amref -Tanzania, kwa kujenga kituo cha muda kwa ajili ya kutoa tiba kwa warahibu wa dawa za kulevya ambacho kimegharibu Sh. milioni 20 za Kitanzania.

"Tumeona tunaweza kufanya huduma hizi kwa gharama nafuu, ninafurahi kuona kwamba zimetumika takribani Sh. milioni 20 kwa ajili ya kutengeneza kituo cha muda kwa huduma za kliniki katika Mkoa wa Tanga," alisema Waziri Ummy.

Waziri Ummy Mwalimu alisema kuwa ilikuwapo haja ya kuwa na kliniki ya methadone kwa Mkoa wa Tanga kutokana na kuwa na waathirika wengi wanaotumia dawa za kulevya, huku mkoa huo ukishika nafasi ya pili ya kuwa na warahibu wengi wa dawa hizo.

"Mkoa wa Tanga unashika nafasi ya pili ya kuwa na idadi kubwa ya watumiaji wa dawa za kulevya, takwimu za mwaka 2016 zinaonyesha Mkoa wa Tanga una watumiaji taribani 5,190 wa dawa za kulevya," alifafanua Waziri Ummy.

Waziri Ummy alisema hadi sasa kuna kiliniki 8 ambazo zinatoa huduma katika maeneo mbalimbali nchini ambapo kwa Mkoa wa Dar es Salaam kliniki hizo zimeanzia katika hospitali ngazi ya mikoa na kushuka chini kwenye hospitali za ngazi ya halmashauri, na kutaja maeneo yatakayofuata kuwa na huduma hizo ni Bagamoyo, Kigamboni, Mbagala, Tegeta pamoja na Magereza Segerea.

Naye Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, James Kaji, alisema wiki hii Tanzania inaungana na mataifa mengine kuadhimisha siku ya kupinga dawa za kulevya ambayo kwa mwaka huu kauli mbinu ni 'tujenge uelewa sahihi kwa tatizo la dawa za kulevya ili kuimarisha mapambano dhidi ya tatizo hilo'.

"Uzinduzi wa kituo hiki ni muendelezo wa vituo vingine nane vinavyotoa huduma nchini ambapo kwa Dar es Salaam vipo vitatu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala na Temeke; Mbeya-Hospitali ya Rufani ya Nyanda za Juu Kusini; Mwanza-Hospitlai ya Rufani ya Sekou Toure; Bagamoyo na Dodoma-Itega" alifafanua Kamishna Jenerali Kaji

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigella, alisema Mkoa wake ni miongoni mwa mikoa yenye idadi kubwa ya shughuli za usafirishaji wa dawa za kulevya na kufanya kuwa na idadi kubwa ya watumiaji ambao hiingia kwenye urahibu wa dawa hizo.

Aliiasa jamii kuepukana na matumizi ya dawa za kulevya, huku akiwaomba kutoa taarifa kwa mamlaka kwa wale wanaojihusisha na usafirishaji na biashara ya dawa hizo.




Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, akivuta pazia kuzindua rasmi bweni la wasichana la Shule ya New Kiomboi ya Wilaya ya Iramba, mkoani Singida juzi, ambapo Benki ya NMB, ilitoa msaada wa vitanda 80 vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10, kwa ajili ya bweni hilo. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Emmanuel Luhahula. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TPN yaishukuru serikali kuwafutia VAT

**Na Beatrice Philemon**

WANACHAMA wa Mtandao wa Mazao ya Jamii ya Mikunde (TPN), wameishukuru serikali kwa kuwasaidia kuondoa tozo ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye mazao ghafi yanayosafirishwa kwa ajili ya kuuzwa katika masoko ya nchi za nje.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Bodi ya TPN, Cosmas Bulala, alipokuwa alizungumza na waandishi wa habari kuhusu sekta ya jamii ya mikunde na jinsi serikali ilivyowasaidia kutatua changamoto zao katika sekta yao ya jamii ya mikunde.

"Kuondoa tozo hii imesaidia kuongezeka kwa masoko ya mazao ya jamii ya mikunde katika masoko ya nje na ushindani wa mazao yetu nje ya nchi," alisema.

Alisema wanachama wa TPN ni pamoja na wakulima, wafanyabiashara, wasindikaji na watoa huduma.

Uamuzi huo ulitangazwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alipokuwa akiwasilisha bejeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Bulala alisema wataongeza mapato kwa wakulima na kuwahamasisha kuongeza uzalishaji zaidi wa mazao haya.

Aliwaomba wakulima waliojikita katika kilimo cha mazao ya jamii ya mikunde nchini walime mazao yao, wahifadhi kwenye kiwango bora ili waweze kupata fedha nyingi katika masoko ya nchi za nje.

"Wakulima wazingatie uhifadhi na ubora wa mazao kwa sababu hivi sasa kuna soko kubwa la maharage, choroko, dengu, mbaazi, kunde na mazao mengine katika nchi za nje," alisema.

Alisema wanaishukuru serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na hatimaye kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara.

Akizungumzia dawa ya kupulizia kwenye mazao inayoitwa 'Methyl Bromide fumigant', alisema tangu serikali ianze kuruhusu matumizi ya dawa hiyo katika mazao ya jamii ya mikunde yanayosafirishwa kwenda katika soko la India, hivi sasa soko lao limekuwa kubwa na wamefanikiwa kuuza mazao ya jamii hiyo yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 150.

# Utekelezaji miradi Kinondoni wamfurahisha Kandege

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Josephat Kandege, amesema ameridhishwa na matumizi ya fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni zilizotumika katika utekelezaji wa miradi ya maedeleo iliyokamilika kwa wakati na viwango.

Alisema manispaa hiyo ni mfano wa kuigwa kwa kuwa imeonyesha nidhamu nzuri kwa matumizi ya fedha zinazotokana na vyanzo vya mapato ya ndani na kwamba miradi ambayo imetekelezwa kupitia fedha hizo inaendana na thamani halisi.

"Kimsingi leo nimemaliza ziara yangu katika halmashauri hii na kikubwa nilikuwa nimelenga kuona fedha zinazokusanywa na halmashauri na namna ambavyo zinatumika katika miradi ambayo inaonekana na kimsingi naomba niwapongeze sana Kinondoni, mnazitendea haki fedha zenu mnazokusanya," alisema Kandege.

Alisema ameridhishwa na kiwango cha barabara zinazojengwa katika halmashauri hiyo kupitia mradi wa DMDP na kuwa kukamilika kwake kutaleta mafanikio kwa wananchi hasa watumiaji wa Barabara ya Shekilango ambayo itaondoa msongamano wa daladala na kuwawezesha wananchi kuondokana na adha ya foleni.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na uongozi wa Rais Dk. John Magufuli na usimamizi mzuri wa Mkurugenzi Aron Kagurumjuli.

Katika hatua nyingine, Kandege ameipongeza Manispaa ya Kinondoni kwa kujenga kituo cha afya katika Kata ya Kigogo kwa kuwa walifanya uamuzi wa busara na kujali wananchi.

"Kinondoni mliona mbali kuweka kituo cha afya pale Kigogo, mlitumia busara ya hali ya juu mkaona ni bora mnunue eneo kwa ajili ya kuwajengea wananchi kituo cha afya," alisema.

Kandege alitembelea Barabara ya Shekilango inayojengwa kwa kiwango cha lami kwa Sh. bilioni 14. 8, mfereji wa Kilongawima uliyopo Jimbo la Kawe kwa Sh. bilioni 3.1 pamoja na upanuzi wa zahanati ya Bunju, mradi unajengwa kwa cha Sh. milioni 600.

# Wenye ulemavu waitwa kugombea Oktoba

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MWENYEKITI wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Michael Mkanjiwa, amewataka watu wenye ulemavu hasa wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu ujao.

Mkanjiwa aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari, na kueleza namna walivyojipanga kuhakikisha wanapata wawakilishi viongozi hasa wanawake wenye ulemavu, ambao watawasemea matatizo na mahitaji yao ngazi ya kitaifa.

Alisema Wilaya ya Kahama inazaidi ya watu wenye ulemavu 3,000, lakini wanaojitokeza kugombania nafasi za uongozi mbalimbali za udiwani na ubunge katika majimbo ya Msalala, Ushetu na Kahama Mjini ni wachache ukilinganisha na waliopo.

"Mwaka 2017 nilijitokeza kugombania nafasi ya ujumbe wa mkutano Mkuu wa Taifa kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilaya na kushinda kwa kupata kura 856 na kuwashinda wasiokuwa walemavu. Hivyo tukijitokeza kugombea tunaweza tukashinda," alisema.

Mkanjiwa aliongeza: "Tunataka uchaguzi huu tupate viongozi wenye ulemavu, ambao watatusemea matatizo yetu hasa viongozi wanawake....Viongzoi wenye ulemavu wanaweza kufanya mambo makubwa kwenye nchini hii ukilinganisha na viongozi wasiokuwa na ulemavu."

Hata hivyo, Mkanjiwa alisema, wengi wao wanashindwa kujitokeza kwenye uchaguzi kugombania nafasi mbalimbali kwa kuogopa kuchekwa na kutoungwa mkono na wananchi kwa madai viongozi wenye ulemavu hawawezi kuwa viongozi wazuri.

Pia, alisema kuwa, kipindi cha nyuma wenye ulemavu walishindwa kujitokeza na kugombea nafasi za uongozi kutokana na kukithiri kwa vitendo vya rushwa ndani ya vyama vya kisiasa, lakini kwa mwaka huu hali imekuwa tofauti na kila mmoja anahaki ya kuwa kiongozi.

Aidha, Mjanjiwa alisema kwa sasa hatua waliyochukua ni kuwaelimisha watu wote wenye ulemavu juu ya umuhimu wa kujitokeza na kugombea nafasi za uongozi pamoja na kuwaelimisha wananchi wengine umuhimu wa kuchagua viongozi wenye ulemavu kuanzia ngazi ya kata hadi wilaya.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akipita jirani na rundo la takataka zilizotelekezwa kwa takribani wiki moja sasa katika kituo cha daladala cha Tabata Segerea, jana, kitendo kinachoweza kusababisha magonjwa ya mlipuko. **PICHA: SABATO KASIKA**.

# Mganga wa kienyeji, wasaidizi wake kizimbani madai ya kubaka

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MGANGA wa kienyeji na wasaidizi wake wawili, wamefikishwa mahakamani wakituhumiwa kumbaka mwanamke, ambaye walitaka kumpatia matibabu.

Wamedai kuwa walifanya hivyo wakidai wametumwa na shetani kuwa hatia hiyo ni miongoni mwa masharti ya kupona maradhi.

Watuhumiwa hao ni Hemed Ali Khamis (24), mtoto mwenye umri wa miaka 16, na mtoto mwenye miaka 15, wote wakazi wa Mikinduni Mgagadu Wilaya ya Mkoani.

Wakisomewa mashtaka na Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Pemba, Asya Ibrahimu Mohamed, alidai mtuhumiwa wa kwanza, Hemedi Ali Khamis, alitenda kosa siku na tarehe isiyofahamika Januari mwaka huu saa 5:00 asubuhi kwenye mabonde ya Mikinduni Mkoani.

Ildaiwa akiwa kama mganga wa kienyeji, alitumia nafasi yake kumbaka mwanamke huyo (40, jina linahifadhiwa) ambaye alitaka kumfanyia matibabu, huku akidai ametumwa na shetani wake kama ni miongoni mwa masharti ya kupona maradhi yake.

Washtakiwa wanadaiwa kutenda kosa hilo kwa siku tofauti. Ilidaiwa mwezi huo huo kwenye mabonde ya Mikinduni, mganga huyo alimbaka mwanamke huyo akiwa na lengo la kutaka kumfanyia matibabu.

Kosa la tatu lilidaiwa kutendwa na mtuhumiwa huyo na wa pili katika siku na tarehe isiyofahamika Machi mwaka huu saa 6:00 mchana katika mabonde ya Mgelele Mikinduni, ambapo walimbaka mwanamke huyo.

Katika kosa la nne, mshtakiwa wa kwanza na wa tatu wanadaiwa mwezi huo huo saa 4:00 asubuhi katika mabonde ya Mgelele, walimbaka mwanamke huyo.

Katika kosa la tano, alilitenda mtuhumiwa namba mbili pekee mwezi huo majira ya asubuhi Mikinduni Mkoani alimbaka mwanamke huyo.

Baada ya watuhumiwa hao kusomewa mashtaka yao, Hakimu wa Mahakama ya Mkoa A Chakechake, Abdul-Razzak Abdulkadir Ali, aliliahirisha shauri hilo hadi Julai 2, mwaka huu.

## Wana-CCM Mtwara waonywa Oktoba

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ally Maulid ambaye ni mlezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Mtwara, amewaonya wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya mkoa huo na wa wilaya zote za mkoa wa Mtwara kutojiingiza kwenye vitendo vya rushwa kwa dhamira ya kutaka kupitisha majina ya wagombea ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 2020.

Aidha, amewataka wanachama wa chama hicho mkoani Mtwara kuachana na tabia ya kujengeana chuki, makundi ikiwamo na kuchafuatana wasifu jambo ambalo halileti afya njema kwa CCM badala yake wanapaswa kuwa kitu kimoja ili kuendelea kukijenga chama hatimaye kiweze kupata ushindi kwenye uchaguzi huo.

Maulid aliyasema hayo wilayani Masasi alipokuwa akizungumza na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa na Halmashauri Kuu ya Wilaya ya Masasi kwenye mkutano maalumu uliowakutanisha wajumbe hao na mlezi huyo.

## Kigoma wahimizwa hadhari ya corona

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

KATIBU Tawala Mkoa wa Kigoma, Rashidi Mchatta, amewataka wananchi wa mkoa huo kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Covid -19 kwa kunawa mikono na maji tiririka pamoja na kuvaa barakoa katika mikusanyiko kwa kuwa nchi jirani bado zina maambukizi ya ugonjwa huo.

Mchatta alitoa rai hiyo jana wakati akipokea msaada wa vitu mbalimbali vya kujikinga na maambukizi ya Covid-19 vyenye thamani ya Sh. milioni 6 kutoka kwa Mratibu wa Shirika lisilo la kiserikali la Bush to Base Solutions mkoa wa Kigoma, Lomayani Komolo, eneo la Mnarani Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Alisema pamoja na Mkoa wa Kigoma kutokuwa na Covid-19, wananchi wanapaswa kujihadhari na ugonjwa huo.

Aidha, alisema mdau huyo ametoa msaada huo kwa sababu shule za sekondari na msingi zitafunguliwa Juni 29, mwaka huu. Aidha, alisema kutokana na shughuli zao zipo kwenye hifadhi ya Mahale Wilaya ya Uvinza, msaada huo utapelekwa maeneo ya Kusini mwa Kigoma ili kusaidia wananchi wa vijiji vinavyopakana na hifadhi hiyo.

Alilishukuru Shirika la Bush to Base kwa msaada huo ambao unahusisha vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa Covid-19 vyenye thamani ya Sh. milioni 6 pamoja na mafuta lita 200 kwa ajili ya kusafirisha vifaa hivyo katika vijiji vilivyopo kando kando ya hifadhi ya Mahale.

## HABARI KITAIFA

# Sekta binafsi kushiriki uibuaji fursa za uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) inatarajiwa kushiriki kwenye kongamano la siku moja mkoani Songwe linalolenga kuwaeleza vijana fursa za kiuchumi mkoani mwao na Tanzania kwa jumla hapo kesho.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa moja ya shabaha kuu za TPSF ni kuhakikisha sekta binafsi ya siku za baadaye inajengwa na vijana wabunifu, wanye kujituma sana na wenye kufanyakazi zenye tija.

“Kama sehemu ya mikakati yetu ya miaka mitano, TPSF kwa kushirikiana na wenzetu wa Mkoa wa Songwe, tumeandaa kongamano la vijana ambalo litafanyika Jumamosi ijayo. Katika kongamano hilo fursa mbalimbali zitaonyeshwa na namna vijana wanavyoweza kuwa sehemu muhimu katika ukuaji wa sekta isiyo rasmi hapa nchini,” alisema Simbeye.

Ametoa wito kwa vijana wa Mkoa wa Songwe kuhudhuria kongamono hilo ili kupata ufafanuzi na maelezo juu ya fursa zilizomo mkoani mwao na ambazo zitawasaidia vijana kujikwamua kiuchumi.

# Waziri Mkuu awaasa wakulima kutokata tamaa kushuka bei

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wakulima wa mazao ya biashara wakiwamo wa ufuta kuendelea na kilimo na kwamba suala la kushuka bei lililotokea kwenye msimu wa mwaka huu lisiwakatishe tamaa.

Amesema serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hilo na kwamba bei ya mazao nchini itaimarika baada ya kuongezeka kwa ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao nchini ili wakulima wawe na masoko ya uhakika na nchi kuuza bidhaa zitokanazo na mazao hayo na si malighafi.

Alitoa kauli hiyo juzi, wakati akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Nachingwea wilayani Ruangwa, mkoani Lindi alipokuwa katika ziara ya kikazi.

“Kushuka kwa bei ya ufuta kusiwakatishe tamaa na kuwafanya muache kulima kwa sababu bei haijashuka kwa zao hilo tu bali na mazao mengine kama chai, tumbaku, kahawa na mazao mengine. Hali hii imetokana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19 ambao umeikumba dunia,” alisema.

Alisema serikali inatarajia kadiri ugonjwa wa Covid-19 unavyoendelea kupungua katika mataifa mbalimbali duniani hali ya bei ya mazao nayo itaimarika, hivyo wakulima waendelee kuwa na subira katika kipindi hiki cha mpito.

Pia, aliwaalika wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza katika viwanda vya kuchakata mazao kwa sababu watakuwa na uhakika wa upatikanaji wa malighafi pamoja na nishati ya kutosha.

Alisema moja ya msisitizo wa serikali ni kuboresha sekta ya kilimo ili iweze kujitosheleza kwa chakula. “Suala la bei ya mazao linapangwa na wanunuzi serikali inasimamia tu.”

Aliwashukuru wananchi wa wilaya hiyo kwa umoja na mshikamano waliompatia katika kipindi chote cha miaka mitano na kuwasisitiza waendelee na ushirikiano huo kwa ajili ya maendeleo ya wilaya yao na taifa.



Mfanyabiashara wa mafagio, akiwauzia wateja wake katika Soko la Ilala, jijini Dar es Salaam jana. Fagio moja liliuzwa kwa bei ya 1,500/-. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Kamusi ya lugha ya alama mbioni

**Na Lucas Raphael,** TABORA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Ave Maria Semakafu, amesema ifikapo Agosti mwaka huu Tanzania itazindua kamusi ya Kishwahili itakayokuwa katika lugha ya alama kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum hasa wenye uziwi kwenye shule za msingi na sekondari.

Alikuwa akizungumza katika uzinduzi wa awamu ya pili ya kuchambua alama na kupiga picha za mwisho ili kuandaa kamusi ya lugha ya alama ya Tanzania kwa ajili ya wanafunzi wenye uziwi iliyofanyika mkoani Tabora.

Dk. Semakafu alisema ili kutimiza lengo la serikali ya kuhakikisha kumusi hiyo inakamilika Agosti mwaka huu na ifikapo mwakani iweze kutumika kwenye shule zenye wanafunzi wenye uziwi.

Alisema usanifishaji wa lugha ya alama Tanzania utasaidia kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi viziwi katika shule za msingi na sekondari.

Alisema hali hiyo itasaidia kuondoa changamoto za kimawasiliano zilizopo kwa kipindi cha sasa, ambapo zinasababisha wanafunzi viziwi kukosa nafasi ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu na hata kukosa ajira na hivyo kushindwa kujikwamu kiuchumi.

Awali Mkurungezi wa Tasisisi ya Elimu Tanzania, Anet Komba, alimweleza Dk. Semakafu kwamba Tanzania inatarajia kupata kamusi bora ya lugha ya alama ambayo kwa kiasi kikubwa itarahisisha kitendo cha ufundishaji kwa wanafunzi viziwi.

Aliushukuru uongozi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Askofu Mihayo (AMUCTA) kwa kutoa eneo la kufanyia kazi na wataalamu mbalimbali wanaoshiriki katika kuhakikisha kamusi hiyo inakamilika kwa muda uliopangwa.

# Halotel yawarahisisishia wateja huduma

**Na Mwandishi Wetu**

MTANDAO wa HaloPesa wenye mawakala zaidi ya 52,000 nchini umewahakikishia wateja wake kupata huduma kwa urahisi zaidi na kujikita kidigitali zaidi kwa kuzindua huduma ya HaloPesa App na kampeni ya #Chillax na HaloPesa App.

Taarifa iliyotolewa na kampuni ya Halotel kwa vyombo vya habari ilisema wateja wanaweza kupakua Halopesa App kupitia simu zao za mkononi (simu janja),

Ilisema App hiyo imetengenezwa kwa ubunifu kwa kuzingatia urahisi wa utumiaji ili kuwapa wateja uzoefu tofauti wanapotumia huduma za HaloPesa App. #ChillaxNa HaloPesa App.

Akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari, Mkuu wa Kitengo cha Biashara cha HaloPesa, Magesa Wandwi, alisema, ‘HaloPesa App’ inampa uhuru mteja kutumia simu janja yoyote kwa kuweka namba yake ya simu na neno la siri na kufanya miamala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutuma pesa kiurahisi na usalama kwa namba ambazo wamezihifadhi kwenye simu zao za mkononi na kufanya malipo ya bidhaa na huduma mbalimbali kirahisi.

Pia alisema wateja wanaweza kuangalia salio bure, kupata taarifa mbalimbali za promosheni, kuangalia viwango vya gharama za kutuma na kupokea pesa.

“Tunafuraha kubwa leo kuwataarifu wateja wote wa Halotel kuwa wakipakua HaloPesa App watajipatia bando la GB1 na dakika 10 za maongezi bure na kutumia wapendavyo ndani ya siku saba,” alisema.



Ukurasa 13

Jina la hospitali hii apewe Mama Maria Nyerere -2

BUFE
IJUMAA JUNI 26, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


Ukurasa 12

**Walima Mpunga, Mahindi Shinyanga walia waingizwe mfumo wa Stakabadhi Ghalani**

# DC Bagamoyo alivyoingilia kati sakata mapato kudoda bandarini





Wafanyabiashara wa Bandari Bagamoyo, wakimsikiliza Mkuu wa Wilaya Zainab Kawawa (katika picha ndogo), alipowatembelea bandarini kusikiliza kero zao hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Yasmine Protace, BAGAMOYO**

MKAKATI wa baadaye kiserikali ni kuangalia namna inavyopandisha hadhi Bagamoyo, kuwa bandari kubwa na ya kisasa.

Huko awali, Bagamoyo ilitumika kwa muda mrefu kama bandari ya asili na mizizi yake inaenda mbali katika historia ya nchi, hadi ilipochukuliwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), kwa mujibu wa mabadiliko ya kisheria kuhusu chombo hicho.

Kwa maana hiyo, kumeambatanishwa na huduma nyingine muhimu za kibandari kama vile kodi, nishati umeme na usalama.

Kwa sehemu kubwa, Bagamoyo imekuwa inapokea na kusafirisha bidhaa kutoka na kwenda katika maeneo jirani ya nchi, ikiwamo Zanzibar.

Hivi karibuni, wafanyabiashara wanaoitumia bandari ya Bagamoyo waliisusa bandari hiyo, kwa madai ya kusumbuliwa kiutendaji, hali inayoelezwa kushusha mapato yake.

Ili kunusuru walakini huo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Zainab Kawawa, alifika mahali hapo na kukutana na wafanyabiashara wanaotumia bandari ili kusikiliza kero zao.

Hapo ndipo walipoibua changamoto kadhaa za kuitendaji, ambazo Mkuu wa Wilaya aliahidi kuzifanyia kazi, huku akiwasihi wafanyabiashara kuendelea tumia bandari kuingiza na kusafirisha bidhaa zao badarini Bagamoyo.

Ni mambo yaliyojiri kupitia mkutano maalum wa Mkuu wa Wilaya na wafanyabiashara wa Bagamoyo wanaotumia bandari ndogo ya Bagamoyo, alipotamka:"Nimesikiliza kilio chenu, naomba msisuse kufanya biashara zenu katika bandari hii."

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara, wanaotumia bandari hiyo, Shaban Khamisi, aliyewawakilisha mwenzake, analalamika kuwa baadhi ya maofisa bandari wamekuwa kero kwa wafanyabiashara kutokana na kauli zisizofaa.

Anataja changamoto nyingine, ni upande wa utoaji risiti zenye kiwango tofauti na pesa wanazolipia huduma na wakati mwingine kutishia kuwapiga wanapofika ofisi za bandari kupata ufafanuzi na huduma.

Baada ya kupokea kero na malalamiko ya wafanyabiashara hao, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, anasema ni kinyume cha kanuni, taratibu, sheria na miongozo ya utumishi wa umma kutolewa lugha chafu kwa wateja.

Zainabu akawataka wafanyabiashara kuhakikisha tuhuma walizowasilisha kwake zina ukweli, kwani mara baada ya mkutano huo Kamati ya Ulinzi na Usalama, ingeanza kuyachunguza kwa ajili ya hatua kuchukuliwa.

"Kitendo hicho kimeingizia serikali hasara kubwa baada ya wafanyabiashara hao kuisusa bandari ya Bagamoyo," analalamika Zainab.

Rai yake kwa wafanyabiashara hao ni kwamba, warudi katika maeneo yao ya kazi kuendelea na shughuli za kiuchumi, kwa juhudi kubwa.

Pia, Zainab ametumia mkutano huo kumwagiza Meneja Bandari ya Bagamoyo Witharo Jared Witharo, kuacha mara moja yale anayoshutumiwa nayo ya ukiukwaji maadili, kanuni, sheria na taratibu za utumishi wa umma.

Zainab anamkumbusha wajibu wake wa kutoa huduma bora kwa wafanyabiashara, ili kurejesha hadhi ya bandari kama ilivyokuwa mwanzo.

Inaelezwa, Bandari ya Bagamoyo imepata mtikisiko mkubwa wa kimapato, baada ya mapato kushuka kutoka Sh. bilioni tatu Novemba mwaka jana hadi Sh. milioni 293.8 mwezi uliopita, kutokana na wafanyabiashara kudaiwa kususa kuingiza mizigo bandarini,

BIASHARA

# Walima Mpunga, Mahindi Shinyanga walia waingizwe mfumo wa Stakabadhi Ghalani

- Wasimulia wanavyonyonywa na wanunuzi
- Wageni wanunua shambani kwa 'bei dezo'
- Kiongozi Ushirika awaahidi 'mambo jikoni'

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MFUMO wa Stakabadhi Ghalani, ni utaratibu ulioanzishwa kisheria wa kutumia mazao kwenye maghala, kama dhamana ya kupata mikopo kutoka asasi za fedha.

Nchini ulianzishwa mwaka 2000 na ukafanyiwa majaribio katika maeneo mbalimbali, hata ukaonyesha tija.

Kabla ya kuanzishwa, wakulima wengi wa mikoa mbalimbali walikuwa wakilima mazao na kuuza kila mmoja kwa bei yake na kusababisha wakulima wengi kutumia nguvu nyingi kwenye kilimo, huku wakipata ujira kidogo kwa kupangiwa bei na wanunuzi.

Hivyo, ni mfumo ulioanzishwa mahususi kwa wakulima wa mazao ya kibiashara, lengo ni wakopesheke katika taasisi za kifedha pale watakapohitaji mikopo mikubwa, pembejeo na dawa na kisha wanauza mazao yao kwa bei zuri, tena wanayoitaka wao.

Kwa mara ya kwanza, mfumo ulianza kwa wakulima wa mkoa wa Mtwara walipolima zao la korosho na wakuza kwa bei nzuri, huku wakiona umuhimu wa kilimo hicho, kila mkulima alikuwa akilima na kuuza kwa bei yake.

Wilaya ya Kahama, imo katika wilaya zinazozalisha mazao ya kibiashara kwa wingi. Hapo inajumuisha tumbaku, pamba, dengu, ufuta, mahindi, mpunga na korosho, iliyoanzishwa hivi karibuni katika Halmashauri ya Ushetu, mkoani Shinyanga.

Halmashauri hizo mbili, zinaongoza kwa kulima tumbaku na pamba na kuziuza kibiashara kupitia Mfuko wa Stakabadhi Ghalan, jambo lililopandisja ngazi kilimo cha mkoa huo kitaifa.

**KILIMO CHAKULA**

Hata hivyo, kuna mazao ya tumbaku na pamba hapo katika Halmashauri za Msalala, Kahama mjini na Ushetu zinakolimwa mpunga na mahindi, kwenye kilimo cha ziada, kwa ajili ya chakula cha familia zao.

Walima mpunga wilayani hapa, wanatumia nguvu nyingi kwenye uzalishaji wa kilimo hicho, lakini wamekuwa wakipangiwa bei na madalali au wanunuzi kutoka nchi za jirani za Rwanda, Burundi na Uganda ambao wanawafuata moja kwa moja mashambani.

Wakulima hao, kilio chao kikubwa ni kwamba kuna ukosefu mkubwa katika kupata bei sahihi ya kuuza mazao yao, hasa mpunga, hali inayowafanya wakulima wa halmashauri wapaze sauti kuomba kujiunga na Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, kama ilivyo kwenye mazao mengine ya korosho.



Walima mpunga katika wilaya ya Kilago, Halmashauri ya Mji Kahama, wakiwa katika mavuno.

> **"Kwa sasa gunia la debe saba la mpunga linauzwa kwa Sh. elfu 35 hadi elfu 40 bei, ambazo hazimnufaishi mkulima. Walanguzi wanatufuata moja kwa moja hadi shambani kununua mpunga badala ya kusubiria mzigo sokoni," anasema Madaha.**

**WAKULIMA MPUNGA**

Mussa Bundala, ni mkulima wa mpunga kutoka kijiji cha Nyanembe, iliyoko katika Kata ya Kilago, ndani ya Halmashauri ya Mji Kahama.

Analalamika wanatumia nguvu nyingi katika uzalishaji, lakini wanakutana na bei ndogo ya mazao yao sokoni, kutoka kwa ama madalali au wanunuzi kutoka nje za jirani.

Bundala anasema, katika msimu huu wamepata mavuno mengi ya zao hilo, ikilinganisha na msimu uliopita, lakini kila sehemu waliyolima zao hilo kila wakulima waanaambulia kidogo.

Bundala anatoa mfano, Kahama bei ya bidhaa zao katika Halmashauri ya Msalala, wanauza debe sita hadi saba za mchele, kwa wastani shilingi 35,000 huku Halmashauri ya Msalala wakiuza 45,000 hadi 60,000.

Bundala anaendelea kuwa, endapo zao hili litaingizwa katika mfumo wa Stakabadhi Ghalani, utawawezesha wakulima kuondokana na ulanguzi holela unaofanywa na madalali, hususani katika kipindi hiki cha mavuno, kwani sheria zitawazuia kumfuata mkulima shambani.



Mkulima wa mpunga kutoka Kata ya Kilago, Halmashauri ya Kahama Mjini, mkoani Shinyanga, Hamisi Mgeja, akionyesha shamba lake. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

**UPANGAJI BEI**

Mwingine, Shika Madaha, anasema wanazalisha mazao ya biashara, lakini suala la upangaji bei unatoka kwa wanunuzi na mwaka mavuno yanapokuwa mengi, bei zinashuka maradufu na kuwakatisha tamaa za kuendelea na uzalishaji wa zao hilo.

"Kwa sasa gunia la debe saba la mpunga linauzwa kwa Sh. elfu 35 hadi elfu 40 bei, ambazo hazimnufaishi mkulima. Walanguzi wanatufuata moja kwa moja hadi shambani kununua mpunga badala ya kusubiria mzigo sokoni," anasema Madaha.

Mkulima, Hamisi Mgeja, anaiomba serikali kuongeza msisitizo katika zao mpunga, kwa kuwakopesha wakulima pembejeo kama ilivyo kwenye tumbaku na pamba, hali inayowadhibiti wageni wanaoingia nchini na kufuata mazao kwa wakulima shambani.

Bundala, anachangia kwa kuiomba serikali kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), kuwaingiza wakulima na kuuza zao hilo kwenye mfumo wa Stakabadhi Ghalani, ili nao wanufaike na bei nzuri.

Anasema, hiyo itasaidia kuondoa wizi katika vipimo unaofanywa na baadhi ya wanunuzi wanaotumia ndoo na magunia makubwa, hali inayowaingiza wakulima wauzaji kupata hasara, ikilinganisha na nguvu waliyotumia shambani.

Bundala anasema wakulima wengi wamekuwa wakiibiwa mazao shambani na madalali, kwa visingizio vya ubovu wa barabara za kusafirisha mazao hadi sokoni au kwenye maghala yao, wakihimiza kuuziwa bei ndogo.

Mgeja anatetea hoja yake, kwamba wao wanaomba kuingizwa kwenye Stakabadhi Ghalani, ili kuondokana na kuibiwa mazao na madalali, sasa wanataka kunufaika na mazao yao kama ilivyo kwa wakulima wa zao la korosho Mtwara.

**RC & WAZIRI**

Wakati wa Mkutano Mkuu wa 24 wa KACU, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alimuomba Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kwamba katika msimu uliopo wa kilimo, wakulima wa mpunga waingizwe katika Mfumo wa Stakabadhi Ghalani.

Anasema, Kahama ina wakulima wengi wa mpunga na viwanda vya kutosha vya kuchakata zao hilo, lakini wakulima wamekuwa wakiuza kwa bei ya hasara, ikilinganishwa na nguvu na rasilimali wanayotumia, hivyo ni vyema wakaingizwa ama kwenye mfumo rasmi wa vyaka vya masingi au Stakabadhi Ghalani.

Aidha, Mkuu wa Mkoa Zainab, alipiga marufuku wanunuzi wa zao hilo kwenda moja kwa moja shambani kufanya biashara na badala yake, wasubiri mazao yafike sokoni, kwani kufanya hivyo kunachangia wakulima kuuza mazao yao kwa bei ndogo tofauti na iliyoko sokoni kwa wakati huo.



Mweyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama, Emmanuel Charahani.

Katika hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alilitolea ufafanuzi kwa kumtaka Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika (KACU), Emanuel Charahani, kuhakikishiwa anapata idadi kamili ya wakulima wa mazao ya kimkakati, kama vile mpunga na mahindi na kuwasajili katika vyama vya msingi.

Anasema, mkulima anapokuwa kwenye vyama vya msingi anaweza kuuza mazao yake ya biashara kwa bei nzuri na kuona umuhimu wa kilimo chake.

**MWENYEKITI KACU**

Emmanuel Charahani, Mwenyekiti wa KACU, anasema serikali kupitia Wizara ya kilimo, ilishatoa maelekezo kuhusiana na kuyaingiza mazao ya kimkakati katika ushirika na kuanzia msimu wa kilimo wa mwaka 2021/22, zao hilo litahamia katika mfumo wa Stakabadhi Ghalani.

Anasema, kwa sasa viongozi wa vyama vya msingi kwenye Halmashauri za Msalala, Kahama Mjini na Ushetu, wanaendelea kutangaza majumbani na kuwasajili, ili kutambua idadi yao na kuwaingiza kwenye vyama vya msingi.

Hata hivyo, Charahani anawataka wakulima wa mazao hayo ya kimkakati, kuhakikisha wanawapatia ushirikiano viongozi wanaopita na kuwasajili ili kuhakikisha katika msimu ujao wa kilimo, kila mkulima awe kwenye vyama vya msingi au mfumo wa stakabadhi ghalani.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Jina la hospitali hii apewe Mama Maria Nyerere -2






**NA JOSEPH KULANGWA**

WIKI iliyopita tuliona uamuzi mbalimbali uliofanywa na Rais John Magufuli. Nini kinafuata? Endelea…

KANA kwamba haitoshi, hivi sasa Hospitali ya Rufani ya Kwangwa, inayojengwa mjini Musoma mkoani Mara, inakaribia kukamilika. Hiyo ni baada ya kuanza kujengwa enzi za Mwalimu Julius Nyerere, katika miaka ya sabini na ikasimama.

Awamu zote za uongozi kitaifa zilipita, bila ya kuigusa. Ikabaki kukaaka magofu.

Hiyo ni ndoto nyingine ya Mwalimu Nyerere, ambayo ikikamilika, utakuwa ukombozi mkubwa sana kwa wakazi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa na hata nchi jirani zilizo kwenye ukanda wa Maziwa Makuu.

Kutelekezwa kwa hospitali hiyo, pengine kulichangiwa pia na kuwapo hospitali nyingine kubwa ya rufaa ya Bugando jijini Mwanza na hivyo waliokuwa na dhamana wakati huo, kuamini kwamba huenda ikawa ni kupoteza fedha kuwa na hospitali nyingine kubwa ya Musoma.

Inawezekana ikawa hivyo, lakini yawezekana pia Mwalimu Nyerere alikuwa na fikra tofauti, akiona kwamba pengine kuwapo hospitali hiyo mjini Musoma, kungeweza kuwasaidia Watanzania, Wakenya, pia kwa Waganda kutokana na imani aliyokuwanayo ya siku moja kuwa na nchi moja ya Afrika Mashariki.

Hivyo mtu akitaja Dodoma kama makao makuu, akataja Stiegler's Gorge na Hospitali ya Kwangwa, atakuwa amemgusa MwalimuNyerere moja kwa moja na atakuwa amefufua fikra chanya za Baba huyo wa Taifa la Tanzania.

Ningetamani kama wangekuwapo marehemu Balozi Paul Ndobho, aliyewahi kuiwakilisha Tanzania kama Balozi nchini Urusi na Mzee Amosi Mutaragara Chirangi (marehemu), aliyekuwa Mwenyekiti wa TANU na CCM mkoa wa Mara, enzi za MwalimuNyerere.

Pia, wote wakiishi karibu na inakojengwa hospitali hiyo, wangeshukuru na kumpa pongezi Rais Dk. Magufuli kwa uamuzi wake huo wa sasa.

Kwa kasi inavyokwenda katika ukamilishaji hospitali hiyo chini ya usimamizi wa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, ni matumaini yangu, muda mfupi ujao itaanza kuwahudumia Watanzania na wenzetu wa nchi jirani.

Kwa kuwa hospitali hiyo ina heshima yake, napendekeza ikikamilika ipewe jina la Hospitali ya Rufani ya Mama Maria Nyerere, kwa heshima ya mama aliyemlea Baba wa Taifa katika kipindi chote cha uhai wake, akipambania heshima ya Watanganyika na Watanzania hadi kifo chake, Oktoba 14, mwaka 1999.

Mapendekezo yangu yamejikita katika heshima ya Mama Maria na mchango wake katikaTaifa hili na ikizingatiwa ni mama ambaye bado hajapewa heshima ya kumbukumbu yeye hadhi, kama ambavyo mume wake ameipata kitaifa na kimataifa.

Ni taasisi, miundombinu au jengo gani hadi sasa lenye jina la Mama Maria Nyerere, ambalo vizazi vijavyo vinaweza kulitumia kumkumbuka mama huyu mpole, mnyenyekevu na asiye na makuu na mwenye mapenzi ya dhati na nchi yake, lakini na Watanzania wenzake? Kwa kurejea kumbukumbu niliyo nayo binafsi, nadiriki kusema hakuna!

Naamini mama huyo akipewa heshima kubwa kama hii akiwa hai, atajisikia faraja sana akiona Watanzania wanavyomthamini na kumheshimu, kutokana na mchango wake huo uliotokana na kuwa karibu na Mwalimu.

Ni vyema, pia Watanzania tukajenga utamaduni wa kuwatambua na kuwaenzi wenza wa viongozi wetu hasa wa ngazi za urais, kwa kuwa mchango wao ndio unaowawezesha kuongoza vizuri na ndiyo sababu tumeendelea kuwa nao kwa vipindi vya miaka kumi , tangu Mwalimu Nyerere alipong'atuka madarakani.

Tumekuwa tukienzi waume zao viongozi marais, kwa kuwapa kumbukumbu hata zaidi ya moja katika mji mmoja, huku wake zao wakisahaulika.

Tungetarajia kusikia taasisi au miundombinu yenye majina ya Sitti Mwinyi, Khadija Mwinyi, Anna Mkapa na Salma Kikwete.

Tuna viwanja vya Ali Hassan Mwinyi, tuna majengo ya Benjamin Mkapa Towers, tuna Benjamin Mkapa Hospital, tuna Taasisi ya Moyo ya JakayaKikwete, madaraja, barabara, shule na kadhalika.

Hata hivyo, hii haizuii kutoa majina kwa taasisi na miundombinu kwa watu, hata wasio ma rais au wake za marais, kwa watu wenye mchango mkubwa katika tasnia zao, tuna watu kama kina Mhandisi Patrick Mfugale na wengineo.

Hivyo basi, tunapokuwa tunaimba kinadharia kuwa palipo na maendeleo ya mwanaume, nyuma yake kuna mwanamama, basi tuonyeshe kwa vitendo nafasi hiyo. Hapo kimsingi ni mwanamke anapewa fursa ya kuenziwa, kama ninavyopendekeza kwa Mama Maria Nyerere. Mungu ampe maisha marefu dada, mama, shangazi na nyanya yetu huyu. Alamsiki!.

**Mawasiliano: Simu: +255 713 410008 na barua pepe: jkulangwa@yahoo.com**

UCHUMI

# Msuguano mkali Marekani, China nani ashike mamlaka Benki Afrika

- Imeshindikana kumng'oa Mkurugenzi
- Marekani kususa? Kicheko kwa Mchina



Dk. Akinwumi Adesina, akisalimiana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Amina Khamis Shaaban, katika Mkutano wa Sita wa Jukwaa la Ushirikiano Kati ya Jamhuri ya Korea Kusini na Magavana wa Nchi za Afrika, Jijini Busan-Korea Kusini.

**Na Nimi Mweta**

MABADILIKO makubwa katika safu ya wanahisa yanatazamiwa kushuhudiwa katika wiki kadhaa zijazo, kutokana na tofauti za kubwa zilizopo kati ya serikali ya Marekani na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinwumi Adesina.

Marekani imeshindwa kuishawishi bodi ya benki hiyo kumchunguza kwa undani Rais wa AfDB na imekuwa ikieleza kutokuwa na imani na sera anazozifuata, licha ya wanahisa wengine na hasa mwanahisa wa kwanza Nigeria, anakozaliwa Rais wa sasa wa AfDB, anayeeleza kuridhishwa na utendaji wake.

Wachambuzi wa habari wanasema, Marekani haitafunika aibu ya kukwama, ila itajitoa.

Suala hilo lilifikia kilele chake mwanzo wa mwezi Juni. wakati bodi ya AfDB ilipoungana na Kamati ya Maadili ya benki hiyo, iliyofanya uchunguzi kuhusu tuhuma za Marekani, dhidi ya Adesina na kuzitupilia mbali hoja zote.

**MZIZI WAKE**

Ni hoja zilizowasilishwa katika bodi hiyo kwa kutumia barua ya Waziri wa Fedha wa Marekani, Steven Mnuchin, aliyetoa madai yanayofahamika na kuorodheshwa, kisha kupigiwa debe na Stephen Dowd, Mjumbe wa Marekani katika Bodi ya AfDB,

Kunatamkwa kuwapo malalamishi kadhaa ikiwemo upendeleo katika uteuzi wa kujaza nafasi katika benki hiyo na kutumia benki kama chombo cha kisiasa, kujipigia debe arudi madarakani, wakati wanahisa wakimchagua rais wa benki hiyo kwa miaka mitano ijayo, mwezi Agosti ijayo.

> **Mchumi huyo ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Benki ya Standard Chartered nchini Uingereza, hivi sasa ni Balozi Maalum anayekusanya misaada kwa Shirika la Kimataifa la Chanjo, kusaidia bara hilo na kupambana na ugonjwa corona.**

Marekani imshahangaikia kuondolewa kwa Dk Adesina, ikashindikana kutokana na wadau wengine kutolikubalia, halafu inapinga kwa nguvu mshindani wake China katika shughuli za benki hiyo, hasa katika kuundwa mfuko wa uwekezaji unaoitwa Jukwaa la Uwekezaji Afrika (AIF).

Hadi kufika mwisho wa mwaka jana, kulishawekezwa Dola za Marekani bilioni 80 fedha zilizoelekezwa katika miundombinu, mwelekeo unaopingwa na Marekani, Nchi hiyo inadai hatua hiyo ya AfDB, imekiuka mpangilio wa majukumu iliyopewa kutekeleza. Hata hivyo, wanahisa wengine walipongeza hatua hiyo.

Wachambuzi wanasema, kutokana na tofautii hizo, haitawezekana kwa Marekani kuendelea kuwa mwanahisa na Mjumbe wa Bodi ya AfDB, hatua iliyochukua sura katika Shirika la Afya Duniani (WHO).

**CHINA VS MAREKANI**

Mwaka jana, Mmarekani huyo Mjumbe wa Bodi ya AfDB, Dowd, aliandika makala ya maoni katika gazeti moja nchini kwao, akieleza masikitiko yake kuwa Adesina, hajaonyesha kujali namna China inavyokuwa na nguvu kubwa katika uchumi wa nchi nyingi za Afrika.

Pia, anaeleza kutoridhishwa kwa Marekani kukosa kura ya veto katika shughuli za benki hiyo ya Afrika, wakati ni mwanahisa wa nne kwa ukubwa, nyuma ya Nigeria, Misri na Ujerumani.

Inavyoelekea, Uamuzi unaochukuliwa na bodi kukubaliana kwa pamoja kisha inapigwa kura, ni hali ambayo Marekani katika mtazamo wa kawaida, ilipaswa iungwe mkono kimtazamo na Ujerumani, kwa mfano AfDB isiwe mwenyeji wa jukwaa hilo.

Anasema, katika uchambuzi huo, msimamo wa Adesina hakuna haja ya kuhangaika na uwepo wa China na nguvu kubwa katika uchumi wa Afrika.

Pia, kutokuwepo Marekani katika nguvu hiyo, unaikera sana nchi hiyo, hata kufikia hatua ya kuunda mifumo mingine ya kimataifa ya kuingiza fedha katika maendeleo ya Afrika, yenye uwezo wa kushindana na AfDB, pamoja na Jukwaa la Uwekezaji.

Ikirejewa mwaka jana, Marekani iliunda kinachopitwa DFC (Development Finance Corporation) kwa mtaji wa Dola za Mareakni bilioni 60.

Baadhi ya wachambuzi wanasema, Marekani ina nguvu kubwa katika Benki ya Dunia, hivyo ikiunganishwa na DFC, itakuwa na nguvu kubnwa zaidi, hoja inayopingwa na baadhi ya wachambuzi.

Marekani inamteua rais wa Benki ya Dunia, lakini sera zake ni tofauti. Baadhi ya wachambuzi nchini Nigeria, wanasema hadi kufikia mwezi uliopita nchi hiyo ilishafikia tamati na itatumia kutoridhishwa kwake na majibu ya Kamati ya Maadili ya Bodi ya AfDB na huenda ni sababu ya kujitoa.

Wako wanaosema, ni hali itakayoiweka shakani AfDB kwa kupungukiwa na mtaji, suala ambalo baadhi ya wadadisi hawaoni umuhimu wake.

Tayari mtaji uliopatikana kutokana na Jukwaa la Uwekezaji utakuwa unazidi wa Marekani katika benki hiyo na kama China hivi sasa siyo mshirika muhimu na bodi inaweza kupitisha kuchukuliwa nafasi kubwa zaidi, kama haitaongeza mtaji wake kufikia iliposimama Marekani.

Suala hilo limeteka hisia za wachangiaji kwenye mtandao wa gazeti la Guardian nchini Nigeria, ambako kuna maumivu kuhusu Marekani, hasa jinsi ilivyomzuia Waziri wa Fedha wa zamani nchini humo, Dk. Ngozi Okonjo-Iweala, kupewa nafasi ya Rais wa Benki ya Dunia.

Mchumi huyo ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Benki ya Standard Chartered nchini Uingereza, hivi sasa ni Balozi Maalum anayekusanya misaada kwa Shirika la Kimataifa la Chanjo, kusaidia bara hilo na kupambana na ugonjwa corona.

Nafasi ya Rais wa Benki ya Dunia, aliyokuwa anaitaka raia huyo wa Nigeria, ilishachukuliwa na David Malpass, Naibu Waziri wa Fedha nchini Marekani na ameshiriki kwa miaka mingi kuunda sera Marekani hasa kuhusu madeni nchi zinazoendelea. Mkasa huu kuhusu Adesina ni mwendelezo wa kutokuelewana kati ya utawala wa Rais Donald Trump nchini Marekani na taasisi kadhaa za kimataifa, na uhusiano wa taasisi hizo na China kila mara unakuwa ni suala la msingi.

Tatizo lililopo sasa ni kwamba, China inataka kuchukua nafasi yake katika uchumi wa kimataifa, pasipo kuwekewa vipingamizi, wakati haifungui milango ya kununua hisa katika mashirika ya umma na benki.

Pia, nchi kama Marekani hadi sasa haina taasisi kama hizo, ila mashirika ya kuratibu sekta tofauti. Inaeleza nguvu za kiuchumi za kampuni za China zinazopata mtaji wowote inazohitaji kutoka serikali ya China, inavuruga ushindani katika kutafuta tenda tofauti nchi nyingi duniani, kwa kutoa bei ya chini kwa kandarasi za ujenzi.



Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinwumi Adesina. **PICHA ZOTE : MTANDAO**





## UVCCM yapinga wanaotumiwa na mabeberu Oktoba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Kheri James, amewataka Watanzania katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu kuchagua viongozi bora na si wanaotumiwa na mabeberu.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akizindua Shina la Wakereketwa wa CCM Chato lililopo Kata ya Uhuru Jimbo la Dodoma Mjini.

Mwenyekiti huyo alisema Watanzania mwaka huu wana jukumu la kuchagua madiwani, wabunge na rais.

"Katika uchaguzi huu hatuendi kuchagua watu tu, tunaenda kuchagua wenye sifa na viongozi watakaotutendea kazi tunayoitaka, tukachague viongozi bora."

"Tukachague madiwani bora, wabunge bora, na Rais si mnamjua kuna bora zaidi ya yeye? Japo nasikia juzi kuna bwana mmoja kutoka huko kijijini kwao anasema yeye atagombea, kama anadhani kugombea ni rahisi gombea tukuone," alisema.

Aliongeza: "Ugombee tukutane boksi la kura kama hujatoka manyoya, hakuna haja ya kuchosha watu, mimi Mwenyekiti wenu wa vijana wa CCM, tumejipanga juu chini ushindi lazima, akija mgombea aliyeletwa na makaburu tutatandika, atakayeletwa na mabepari tutatandika, atakayeletwa na wabebaishaji tutatandika."

Mwenyekiti huyo alisema kwa kuwa hoja na sababu wanazo na Watanzania wapo tayari kuichagua CCM.

"Kuna mwingine anasema ndani ya CCM ana vigogo sita wanaomuunga mkono, chama hiki hakina vigogo wala vijiti, chama ni cha wanachama, kama kuna vigogo wanakudanganya kukuunga mkono kwamba utafika popote wewe na vigogo vyako wote chali hamtapita popote," alisema.

Kuhusu kamata kamata ya wapinzani, mwenyekiti huyo alishauri viongozi kutowakamata kwa kuwa wapinzani wanatumia fursa hiyo kutafuta umaarufu.

"Mwaka huu kutakuwa na kelele nyingi tusiwape umaarufu wanalazimisha Watanzania wawaonee huruma, kwa watu wanadhani kupiga kelele kuna badili kitu na kutengeneza mazingira ya kuwa Tanzania si salama wakati ni uongo," alisema bila kufafanua kauli yake.

Naye Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema wana-Dodoma wapo tayari kufanya maajabu ifikapo Oktoba 2020 kwa kusimika mafiga matatu ya CCM yaani madiwani, wabunge na Rais.

"Naomba nifikishie salamu kwa Rais Magufuli kuwa wana-Dodoma wanashukuru kwa kuleta maendeleo makubwa, hivyo shukrani zetu ni kufanya maajabu makubwa ya kumrudisha Magufuli kwa kumpa kura za kutosha kwa asilimia 100 pale itakapofika Oktoba 2020," alisema Mavunde.

Aliahidi kuboresha miundombinu katika shina hilo ili wanachama katika shina hilo wakae na kupanga mipango ya maendeleo.

# Wakulima wa ufuta wapewa unafuu

**Na Augusta Njoji,** BAHI

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewaruhusu wakulima wa zao la ufuta mkoani humo kuuza sehemu yoyote wanayoona bei inafaa kutokana na kuporomoka kwa bei kwenye minada.

Awali, Wizara ya Kilimo ilitangaza katika msimu wa mwaka 2019/20 zao hilo litauzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Hata hivyo, kutokana na mwenendo wa baadhi ya minada bei ya zao hilo kuporomoka siku hadi siku, wakulima wa mkoa huo walilazimika kuiomba serikali kuingilia ili kuwepo na bei yenye tija kwao.

Akitoa maelekezo hayo jana wilayani Bahi, Dk. Mahenge alisema maamuzi hayo yametokana na kuporomoka kwa bei katika mnada ulioendeshwa Juni 24, mwaka huu, ambapo bei ilishuka kutoka Sh. 1,931 kwenye mnada wa Juni 2, 2020 hadi Sh. 1,250 kwa kilo moja.

Alisema kabla ya kufikia uamuzi huo alikutana na wafanyabiashara na wakuu wa wilaya wote na kuagiza kuanzia sasa, mwananchi yeyote ambaye bado ana ufuta nyumbani, aende akauze anakoona yeye inafaa.

"Hakutakuwa tena na hii zuia zuia isipokuwa tu utatulipia ushuru wetu kwenye geti, mmenielewa ndugu zangu waambieni na wananchi wote kwamba muda uliobaki serikali imeamua kuwaachia wananchi, lakini kama ipo chini ya tani moja unapeleka bila malipo ikizidi tani moja unalipa ushuru," alisema.

Alitaja sababu tatu zilizosababisha kushuka kwa kasi kwa bei ya zao hilo ni athari za ugonjwa wa corona, ambapo wanunuzi wakubwa duniani nchi zao hazijafungua mipaka yao, hivyo imekuwa vigumu kupeleka ufuta katika nchi hizo.

"Sababu ya pili, Dodoma huwa ya kwanza kuanza kuvuna ufuta, lakini kutokana na mvua nyingi zilizonyesha mwaka huu mavuno yalichelewa kuanza na wakulima wakajikuta wanaanza kuvuna mwezi Mei na Juni ilhali mikoa ya kusini nayo ndiyo msimu wa kuvuna zao hilo," alisema.

Pia alisema nchi za Malawi na Ivory Coast nazo ndiyo msimu wa mavuno hivyo, kufanya ufuta kuwa mwingi sokoni.

"Sababu ya tatu ya kushuka kwa bei ya zao hilo ni uzalishaji wa ufuta ulikuwa mkubwa kwani wakulima wamevuna vizuri kwa kuwa mvua zimenyesha vizuri na za kutosha," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema katika mnada uliofanyika Juni 24, 2020 kwa dakika 15 wilaya hiyo ilikuwa na tani 78.2, ambapo bei ya mnunuzi aliyejitokeza alinunua kwa Sh.1,250 kwa kilo moja jambo ambalo halikuwaridhisha wakulima na kuamua kutouza shehena hiyo.

"Kama kiongozi baada ya kuona hali inakuwa mbaya nikaamua kuchukua hatua kwa kushirikiana na wakulima kutafuta mnunuzi nje ya mnada na ambapo tumempata na atachukua mzigo huo kwa Sh. 1,400 na wakulima wameridhia," alisema.



Mchuuzi wa ndizi, akipanga biashara yake pembezoni mwa barabara ya Soko Kuu la Majengo, jijini Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wake. **PICHA: PETER MKWAVILA** .

# Vyama vyatakiwa kuwapa kipaumbele wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VYAMA vya siasa nchini, vimetakiwa kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu katika nafasi za ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Shirika la Watu wenye Ulemavu (TASODEFA) mkoani Dodoma, Paul Mahinyila, alipokuwa akizungumza na waandishi habari.

Mahinyila alisema hali hiyo itasaidia kuwaondolea hofu ya kutojitokeza kugombea nafasi hizo.

Alisema kuwa vyama vya siasa kwenye uchaguzi wa 2020, ni muhimu wakatoa kipaumbele kwa wagombea wenye ulemavu ili kushiriki kwa wingi katika kinyang'anyiro cha nafasi ya ubunge na udiwani.

Alishauri watu wenye ulemavu, wenye sifa kujitokeza kwa wingi, badala ya kuwa na hofu ya unyanyapaa uliopo miongoni mwa jamii.

"Kutokana na hofu hiyo, tunahitaji jamii iwe na mtizamo chanya juu ya watu wenye ulemavu, hivyo wakiaminiwa na kupewa nafasi hizo wanaweza, ukizingatia kuwa mfano upo wazi rais wetu kwenye serikali amewaweka viongozi wenye ulemavu," alisema.

Naye Mjumbe wa Shirika, Wema Hassan, alitoa wito kwa wanawake wenye ulemavu na wenye sifa za kuongoza kujiamini kwa kujitokeza kwa wingi ili wagombea nafasi hizo.

"Wanawake msijirahisishe kwa ajili ya kutaka kupewa upendeleo, mjiamini kwa kuwa wapo wenye uwezo mkubwa wa kuongoza nafasi hizo," alisema.



HABARI MBEYA



Mkuu wa Magereza Mkoa wa Mbeya, Mathias Mkama (kulia), akipokea msaada wa vifaa vya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona kutoka kwa Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boaz, jijini humo jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**.

# RC aagiza hoteli ya askari anayedaiwa kuua kufungwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameagiza kufungwa hoteli ya askari polisi John Kaijage, anayedaiwa kumuua dereva bodaboda, Erasto Mwalwega (29), kwa kupigwa na kitu butu kichwani akimtuhumu kumuibia mablanketi na mashuka ndani ya hoteli yake.

Pia ameagiza uchunguzi wa kifo cha Mwalwega ukamilike haraka ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya askari huyo na wenzake watatu wanaodaiwa kuhusika na mauaji hayo.

Chalamila alitoa agizo hilo jana nyumbani kwa marehemu eneo la Nzovwe wakati wa shughuli za kuuaga mwili wa marehemu Mwalwega ambaye tangu afariki dunia Juni 21, mwaka huu, ndugu zake waligoma kuchukua mwili na kuuzika wakishinikiza haki itendeke na waliohusika na kifo hicho kwa makusudi wakamatwe.

"Ni aibu kwa askari wa Jeshi la Polisi ambaye nchi imekuamini kulinda raia na mali zao kuhusika na mauaji ya raia ambaye kwa mujibu wa maelezo hakuwa na hatia kwa sababu hakuthibitisha marehemu kumuibia mashuka yake, ninaomba adhabu ya huyu bwana iwe kali na fundisho kwa polisi wengine wanaojichukulia sheria mikononi, vilevile naagiza hoteli yake ifungwe mara moja isitoe tena huduma," alisema Chalamila.

Alisema alipata taarifa kutoka kwa msamaria mwema kuhusu polisi kumuua dereva bodaboda na kumuagiza Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, kumkamata pamoja na wenzake watatu.

Aliwashauri wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kutokana na mali na utajiri walionao na kuamua kugharimu maisha ya wengine bila sababu na kuwasisitiza kuwa na hekima ya Mungu ili awasaidie kuwa na nidhamu ya fedha zao.

Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, alisema uchunguzi wa awali umebaini Polisi Kaijage kuhusika na mauaji hayo na kuomba haki itendeke ili iwe fundisho.

Vilevile aliwaomba wafiwa kuwa wastahimilivu katika kipindi hiki kigumu na kuwasihi wazike mwili wa marehemu huku wakisubiri hukumu kutolewa na mahakama.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema hatua za kinidhamu zilichukuliwa dhidi ya polisi huyo na ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria za Mahakama na Jeshi uchunguzi utakapokamilika.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Ilembo Kata ya Iwambi, Daud Dule, alikanusha marehemu kuhusika na wizi wa mashuka na mablanketi kama inavyodaiwa na mmiliki wa hoteli hiyo.

Mwili wa marehemu Mwalwego uliagwa jana nyumbani kwao eneo la Nzovwe na kusafirishwa Rungwe kwa maziko.

# Wafungwa waombewa msaada kujikinga corona

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Magereza Mkoa wa Mbeya, Mathias Mkama, amewaomba wadau kuendelea kutoa misaada ya hali na mali kwa ajili ya kuwasaidia wafungwa na mahabusu waliopo kwenye Gereza la Ruanda kukidhi mahitaji yao.

Mkama alitoa ombi hilo jana wakati akipokea misaada ya vifaa mbalimbali vya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19 ambao kwa sasa umepungua nchini.

Alisema bado kuna uhitaji mkubwa wa sabuni, ndoo, mafuta na nguo kwa wafungwa na mahabusu katika gereza hilo kwa wafungwa ambao ndugu zao wako nje ya mkoa.

Alisema bado vifaa vya kujinga na corona havitoshi kutokana na wafungwa na mahabusu kuingia mara kwa mara na kufanya vilivyopo kutotosheleza.

Akipokea msaada wa vifaa hivyo kutoka kwa Taasisi ya Tulia Trust, Mkama alisema taasisi hiyo ni miongoni mwa wadau wanaosaidia mahitaji ya vitu mbalimbali kwa wafungwa kama mavazi, sabuni na mafuta.

Akikabidhi misaada hiyo, Meneja wa Taasisi hiyo, Jacqueline Boaz, alisema taasisi yake iliahidi kutoa vifaa vya kujikinga na corona kwenye maeneo mbalimbali ya mikusanyiko ikiwamo gerezani ili kuepukana na ugonjwa huo.

Alisema tayari maeneo mengi yamenufaika na hadi sasa Sh. milioni 10 zimetumika kununulia mahitaji mbalimbali kuboresha sekta ya elimu, afya na huduma nyingine za kijamii ikiwamo vya mapombano dhidi ya corona.

# CCM yatahadharisha wanaojiunga kwa kufuata mkumbo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewataka watu wote wanao omba kujiunga na chama hicho kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu kuanza kuijua itikadi na imani ya chama kabla ya kukabidhiwa kadi za uanachama badala ya kufuata mkumbo au kushawishiwa bila kuelewa misingi ya chama hicho.

Rai hiyo ilitolewa na Katibu wa Itikadi, Siasa na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, mkoani hapa wakati wa kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa nyumba ya Katibu wa Umoja wa vijana wa chama hicho wilayani Mbeya mjini inayojengwa katika kata ya Itezi.

Alisema kipindi hiki kinahitaji umakini ndani ya chama kwa kuhakikisha wote wanaotangaza nia ya kujiunga na CCM kuhakikisha wanaamua wenyewe kwa hiari yao bila kuwapo kwa msukumo wa madaraka au ushawishi wa mtu fulani.

Alisema ni muhimu chama kuweka wazi matakwa yake kwa wote waliopendezwa na kazi nzuri zinazofanywa na viongozi wa CCM akiwamo Rais Dk. John Magufuli na kuamua kumuunga mkono, lakini wasifuate mkumbo ili baadaye wasijekujilaumu.

"Tunaendelea kuwapokea wanachama wapya kila kuitwapo leo na hili linadhihirisha kuwa sasa chama kinakubalika kutokana na utendaji kazi wake nawasihi mnaojiunga na chama hiki fuateni misingi na kanuni na sio mkumbo chama kinaendeshwa kwa misingi na kanuni hata wanaotaka kugombea lazima tuwachunguze na kuwafuatilia," alisema Polepole.

Aliwatahadharisha watiania ya ubunge na udiwani kutulia kuachana na masuala ya hongo kwa wanachama kwa kuwa chama kimeweka waangalizi kila eneo hivyo atakayebainika jina lake litakatwa hata kabla ya mchakato.

Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, aliwataka vijana kuendelea kujitathmini na kukienzi chama kwa kuwa ndicho kimewaletea maendeleo.

Akizungumzia mradi wa ujenzi wa nyumba hiyo ya Katibu, Steven Shija, alisema kikwazo kinachowakabili kwa sasa ni rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi huo ambazo ni Sh. milioni 27 ili kukamilisha mradi huo.

# Madawati kusaidia kuleta maendeleo sekta elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrisa Muslim Hija, amesema upatikanaji wa madawati katika shule mbalimbali kutasaidia kuleta maendeleo zaidi katika sekta ya elimu nchini.

Akizungumza wakati wa kukabidhiwa madawati ya Shule ya Msingi Chaani, yaliotolewa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mkoa wa Kaskazini Unguja, alisema madawati hayo yatasaidia kupunguza tatizo la muda mrefu la ukosefu wa madawati katika shule hiyo.

Dk. Idrisa aliwataka wananchi kuzitumia fursa zitokanazo na miradi inayopita katika jamii kwa kujipatia maendeleo katika maeneo yao ili taifa lipige hatua ya kufikia uchumi wa kati.

Akizungumza wakati akimkabidhi madawati hayo, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mustafa Aboud Jumbe, alisema mradi wa ujenzi wa barabara iliyopitia Chaani, ulitakiwa kuchangia maendeleo ya huduma za kijamii na hivyo ikakubaliwa kutengeneza madawati kwa shule hiyo kutokana na kuonekana kutokuwa na huduma hiyo.

Naye Mwalimu wa shule hiyo, Asha Haji, aliishukuru Wizara ya Ujenzi kwa kupunguza tatizo la madawati na kuiomba Wizara ya Elimu kufanya uwezekano wa kuwajengea uzio ili kuimarisha ulinzi wa madawati hayo pamoja na vitu vingine vya thamani.

Kwa upande wake fundi seremala wa madawati hayo, Sultan Abdalla, aliwashauri walimu kuwasimamia wanafunzi kwa kuyatunza madawati hayo ili yadumu na kuwasaidia na vizazi vijavyo.

Kwa upande wao wanafunzi walisema ni faraja kwao kupata madawati hayo ambayo yataondoa tatizo la kukaa chini.

Jumla ya madawati 400 yamekabidhiwa kwa shule hiyo yaliyogharimu Sh. milioni 200.



Walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Hamamni, Mjini Unguja, wakifurahi baada ya kukabidhiwa vifaa vya kujikinga na mambukizi ya virusi vya corona kutoka uongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tawi la Shangani, juzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA.**

# SMZ: Mfumo wa ugatuzi umeleta ufanisi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema kuwapo kwa mpango wa ugatuzi kufikisha huduma muhimu za jamii kwenda moja kwa moja kwa wananchi, kumeleta ufanisi na wananchi kupata ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili ikiwamo huduma za elimu na afya.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Haji Omar Kheir, wakati akiyavunja Mabaraza ya Madiwani kwa ajili ya kupisha uchaguzi mkuu, Oktoba, mwaka huu.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya ugatuzi huduma za elimu ya msingi zimepata mafanikio ikiwamo uandikishaji wanafunzi wa elimu ya msingi na maandalizi kufikia asilimia 100.

Alisema mafanikio hayo yamefikiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na wazazi kuhamasika kupeleka watoto wao shule baada ya serikali kufuta ada zote walizokuwa wakitozwa.

"Nawapongeza madiwani wetu ambao walikuwa miongoni mwa watendaji waktekeleza mpango wa ugatuzi kufikisha huduma muhimu za jamii kwenda moja kwa moja kwa wananchi..." alisema.

Aliwataka madiwani watakaochaguliwa katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, kujikita zaidi kwenye ukusanyaji wa mapato.

"Moja ya changamoto kubwa iliyojitokeza katika mabaraza ya madiwani ni kushindwa kufikia malengo katika ukusanyaji wa mapato ambayo yalitengwa katika bajeti ya mabaraza hayo," alisema.

Naye Meya wa Zanzibar, Saleh Juma Kinana, aliyataja miongoni mwa malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa kwa upande wa mabaraza ya madiwani baada ya uchaguzi mkuu ni kujikita katika ukusanyaji wa mapato.

Alisema uchunguzi umeonyesha kwamba bado vipo vyanzo vingi vya mapato ambavyo havijadhibitiwa vizuri, huku vikipoteza mapato hayo kwa kiwango kikubwa.

"Tumejipanga katika mabaraza ya madiwani yanayokuja baada ya uchaguzi mkuu tutaweka kipaumbele cha ukusanyaji wa mapato katika vyanzo mbalimbali," alisema.

Diwani Thuwaiba Jeni, aliyataka mabaraza ya madiwani yanayokuja kujikita katika kutekeleza dhana ya ugatuzi kufikisha huduma muhimu za kijamii kwenda serikali za halmashauri.

"Mabaraza ya Madiwani yamefanya kazi zake vizuri, lakini tunatakiwa kuongeza nguvu na ubunifu katika ukusanyaji wa mapato ili kuyafikia malengo ya ugatuzi na kufikisha huduma muhimu kwenda katika serikali za mitaa na halmashauri zake," alisema.

Mabaraza ya madiwani yaliyovunjwa yamewajumuisha madiwani wa kuchaguliwa na wananchi katika majimbo ya uchaguzi pamoja na kuteuliwa wapatao 111.

# Z'bar yakamilisha udhamini wa JPM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZOEZI la kumdhamini Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais John Magufuli, limekamilika katika mikoa mitano ya Zanzibar, huku wanachama wakiwamo vijana, wazee na wanawake wakijitokeza kwa wingi na kuonyesha imani kubwa ya uongozi wake katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Kusini Unguja, Hassan Mrisho, aliwapongeza wanachama waliojitokeza kutoka Wilaya ya Kati na Kusini kwamba wamejenga matumaini makubwa ya maendeleo katika kipindi cha miaka mitano ijayo cha uongozi wa Rais Magufuli.

Mrisho alisema kwa upande wa Zanzibar, wanachama wamejenga imani katika kipindi cha uongozi wa miaka mitano huku amani na utulivu ukiimarika katika kipindi hicho na kutoa nafasi ya wananchi kufanya shughuli za maendeleo na uchumi.

"Wananchi wamejitokeza kwa wingi kumdhamini Mwenyekiti wa CCM Taifa katika kuwania nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano... matumaini yetu makubwa ni kupata maendeleo makubwa," alisema.

Baadhi ya wanachama wa CCM waliomdhamini mgombea wa CCM katika kinyang'anyiro cha Rais wa Jamhuri ya Muungano Dk. Magufuli, walisema wameridhika na utendaji wa kazi wa kiongozi huyo katika kipindi cha miaka mitano, huku matumaini yao ni kupiga hatua zaidi katika kipindi cha miaka mitano mingine ijayo.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ame, aliyeongoza zoezi hilo katika mkoa huo, alisema chama kimeridhishwa na uongozi wake na anastahili kuiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ya kiuchumi.

"Sisi wanachama wa CCM tumeridhishwa kabisa na uongozi wake wa miaka mitano ambao umejikita katika kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na maendeleo," alisema.

Kwa upande wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mwenyekiti wa chama, Yussuf Ali Juma, aliwapongeza vijana wa chama hicho kwa kujitokeza kwa wingi kumuunga mkono Rais Magufuli kwa kumdhamini na kujaza fomu za urais.

"Najua vijana mmejitokeza kwa wingi kumuunga mkono Rais Magufuli kwa sababu amefanya kazi kubwa katika kuwanyanyua vijana nafasi za uongozi wa nchi," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDAYA YA UHAMIAJI**

**OMBI LA URAIA WA TANZANIA**



Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni ZIMBABWE. Nchi atokayo ni ZIMBABWE. Yupo hapa nchini tangu 2019. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb Na. DN. 352803

115789402

**KUPOTEA KWA VYETI**



**BARAKA DAFFA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0139-0043** kilichotolewa na MTWARA TECHNICAL SEKONDARI mwaka 2011. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0140-0561 kilichotolewa na MZUMBE SEKONDARI mwaka 2014. Academic Transcript yenye namba **T/UDOM-STR/2015/19105** iliyotolewa na Dodoma University mwaka 2018. University Certificate yenye namba T/UDOM-STR/2015/19105 iliyotolewa mwaka 2018. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **IRI/IRI/RB/434211/2020.**

115788402

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS IMMIGRATION DEPARTMENT
Telegram: IMMIGRATION
Simu 027-250369

REGIONAL IMMIGRATION OFFICE,
S.L.P.236,
ARUSHA.

DATE : 16/06/2020

**APPLICATION FOR CITIZENSHIP**

**Notice is hereby given that:**



**Mrs CATHERINE MORIO KINABO**

Whose photograph is provided above,is applying to the Minister for Home Affairs for Tanzania citicenship.Her Nationality at present is KENYAN. The Country of Origin is KENYA. Her Occupation is HOUSE WIFE. Her Employer/Business/Adress is OLASITI,ARUSHA .She has been in this Country since 2014 apart from ARUSHA Region .She has also resided in ARUSHA Region .

That any person who knows any reason why Citizenship should not be granted to the applicant,should send a written and signed statement of facts to the Commissioner General of Immigration Services,P.O.BOX 512 DAR ES SALAAM. Using Ref.No. ……..and DN/……….

……………………………………………………

**FOR :COMMISSIONER GE
NERAL OF IMMIGRATION
SERVICES.**

115789202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo:
MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;166/2020**

**Ombi la CONSEPTA TOBIAS MPOLO
Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu
ALLY HASSAN KHAMISI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 09/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 25/06/2020.

115789002

**PLOTS FOR SALE IN DODOMA**

**LARGE SURVEYED PLOTS ARE AVAILABLE FOR IMMEDIATE SALE.**

IDEAL FOR LARGE BUSINESSMEN AND/OR LIVESTOCK KEEPERS.

CALL AND/OR TEXT THROUGH PHONE NO

**0762840928.**

***(NO MIDDLEMEN).***

11579002

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**HENRY APOLINARY RWEMELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **NISSAN DATSUN** yenye namba za usajili **T 677 CDP** Chassis Na **LPD22000067,** Engine Na.**KA2Q1Q2184.** Yeyote atakayeyeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**KAG/KAI/RB/379213/2020.**

115788702

**KUPOTEA KWA CHETI CHA UANACHAMA WA TANZANIA INVESTMENT CENTRE**

**WS RISK AND PROTECTIVE SERVICE:**

Inatangaza kupotea kwa Certificate of Incentives. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**DAR/OST/480699/2020**

115788602

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Bei ya mafuta Zimbabwe yapanda mara mbili

**HARARE, Zimbabwe**

BEI ya mafuta nchini Zimbabwe imepanda hadi asilimia 152 baada ya serikali kuondoa kiwango maalum kilichowekwa tangu mwezi Machi.

Mara ya mwisho nchi hiyo ya kusini mwa Afrika ilishuhudia ongezeko la juu la bei la mafuta, Januari mwaka 2019, kulizuka maandamano yaliyokuwa na ghasia, kusababisha zaidi ya watu 17 kuuawa baada ya ukandamizaji uliofanywa na majeshi ya usalama.

Zimbabwe tayari inapitia mzozo mbaya wa kiuchumi katika kipindi cha muongo mmoja, kukiwa na ughali wa maisha wa kiwango cha juu, ukosefu wa dawa na chakula.

Bei ya mafuta imepanda kwa fedha za Zimbabwe 71.62 sawa na dola za Marekani 1.25 kwa lita.

**DW**

**Mara ya mwisho nchi hiyo ya kusini mwa Afrika ilishuhudia ongezeko la juu la bei ya mafuta, Januari mwaka 2019, kulizuka maandamano yaliyokuwa na ghasia, kusababisha zaidi ya watu 17 kuuawa baada ya ukandamizaji uliofanywa na majeshi ya usalama.**

# Maji ya chumvi kufanyiwa utafiti tiba ugonjwa corona

**EDINBURGH, Scotland**

WANASAYANSI bado wanahangaika kupata tiba ya ugonjwa wa virusi vya corona. Watafiti nchini Scotland wamenza majaribio ya maji ya chumvi kama tiba ya ugonjwa huo.

Utafiti wa awali ulionesha kwamba dawa za kutengenezwa nyumbani zinaweza kusaidia kupuguza makali ya dalili za virusi vya corona kama ilivyo kwa homa.

Utafiti huo ulionesha kwamba watu wanaosukutua na kusafisha pua zao kwa maji ya chumvi, kikohozi kinapugua, kubana kwa mbavu kunapungua huku wagonjwa wakionekana kupona kwa haraka.

Wanasayansi wa Chuo Kikuu cha Edinburgh watachunguza ikiwa dawa hiyo pia inaweza kusaidia watu waliopata maambukizi ya virusi vya corona.

Utafiti huo kwa sasa hivi unasajili watu wenye dalili za ugonjwa wa corona ambao wamethibitishwa kupata maambukizi.

Utafiti wa awali ulisajili watu wazima ambao wamebainishwa kuwa na maambukizi katika mfumo wa juu wa upumuaji kwa siku mbili kulikochukuliwa kama homa.

Watu hao waligawanywa kwenye makundi mawili huku kundi la kwanza likitakiwa kusukutua na kusafisha njia ya pua kwa maji ya chumvi wakati wanahisi kufanya hivyo.

Kundi lingine likawa linatibu homa hiyo kwa njia ya kawaida.

Washiriki wote waliweka kumbukumbu ya dalili zao kwa wiki mbili. Pia walipimwa kuangaliwa kiwango cha virusi hivyo vya homa ndani ya pua zao.

Watafiti hao walisema waliokuwa wakisafisha njia ya pua na kusukutua kwa maji ya chumvi, homa yao ilikuwa ya muda mfupi, na kupunguza uwezekano wa kusambaa hadi kwa familia zao.

Walisema watu hao walipona haraka huku wakiwa na uwezekano wa chini wa kutumia dawa zinazouzwa kwenye maduka ya dawa.

Mkurugenzi wa Chuo Kikuu cha Usher, Profesa Aziz Sheikh, alisema: "Sasa hivi tunaingia kwenye utumiaji wa maji ya chumvi kwa waliothibitishwa kupata maambukizi ya ugonjwa wa corona, ni matumaini yetu kwamba yataonesha matokeo chanya ya kupunguza athari za usambaaji wa maambukizi".

Aliongeza: "Kinachohitajika ni chumvi, maji na kuelewa mchakato wa namna mchanganyiko huo unavyotengenezwa. Unastahili kufanya kazi, ikiwa utaonesha ufanisi, itakuwa njia rahisi isiyo na gharama na yenye kutekelezeka sehemu yoyote ile"

***BBC***



Askari wa Urusi akiwa katika gwaride kwenye Uwanja Mwekundu mjini Moscow, katika sherehe ya kuadhimisha miaka 75 tangu jeshi la Kisovieti maarufu kama "Red army" kuishinda Ujerumani.**PICHA: REUTERS**

# Walinzi wa Rais Trump watakiwa kujitenga

**WASHINGTON, Marekani**

WALINZI wawili wa Rais wa Marekani, Donald Trump, wametakiwa kujitenga baada ya kupata maambukizi ya virusi vya corona, vyombo vya habari vya Marekani vimesema.

Imeelezwa kuwa walinzi hao walikuwa katika mkutano wa kisiasa wa Rais Trump katika Jiji la Tulsa.

Mbali na walinzi hao, watu sita waliokuwa katika timu yake ya kampeni nao walipata maambukizi ya virusi vya corona kabla ya mkutano huo, huku wengine wakithibitishwa kupata maambukizi baada ya mkutano.

Idara hiyo ya usalama haikusema wafanyakazi wangapi wamepata maambukizi au wanajitenga.

Gazeti la Washington Post limesema watu sita waliothibitishwa kuambukizwa corona kabla ya mkutano huo walikuwamo walinzi wawili wa Rais Trump.

Wote hao walihudhuria mkutano wa kupanga kitakachofanyika Ijumaa pamoja na walinzi wengine na maafisa, ambao waliendelea kutekeleza majukumu yao hata baada ya matokeo ya vipimo kutolewa.

Ofisa mmoja wa usalama aliiambia Shirika la utangazaji la CNN kwamba idadi ya maofisa walioko karantini ni ndogo.

Msemaji wa Idara ya Usalama, Catherine Milhoan alisema shirika hilo liko tayari kukabiliana na hali yoyote huku wafanyakazi wake wakitekeleza majukumu yao kama inavyohitajika.

"Dhana yoyote inayoashiria kwamba idara hii kwa namna fulani haikuwa tayari au imeshindwa kutelekeleza malengo yake itakuwa sio sahihi," alisema Milhoan.

CNN pia ilinukuu barua pepe za ndani zinazoonesha kuwa maofisa wa idara hiyo walikuwapo kweye misafara ya rais, kwa sasa hivi ni lazima wapimwe virusi vya corona kati ya saa 24 hadi 48 kabla ya kuelekea sehemu nyingine kutekeleza majukumu yao.

Watu waliohudhuria mkutano huo hawakuhitajika kuvaa barakoa au kufuata kanuni ya kutokaribiana lakini walihitajika kupimwa kiwango cha joto la mwili.

Pia walihitajika kusaini hati ya sheria inayolinda kampeni ya Rais Trump kuwajibishwa iwapo mtu ataugua.

Kulingana taarifa iliyotolewa na Idara ya Zimamoto ya Tulsa, takriban watu 6,200 walihudhuria mkutano huo wa kisiasa - theluthi moja ya nafasi ya eneo la tukio.


Wakati huohuo, miji ya New York, New Jersey na Connecticut imetaka watu wote wanaosafiri kutoka maeneo yenye maambukizi ya juu ya virusi vya corona kujiweka karantini kwa siku 14.

Majimbo yaliyoathiriwa ni Alabama, Arkansas, Arizona, Florida, North Carolina, South Carolina, Texas na Utah.

Chuo kikuu cha Washington kinabashiri kuwa idadi ya vifo Marekani itakuwa 180,000 kufikia Oktoba - au 146,000 ikiwa asilimia 95 ya raia wa Marekani watavaa barakoa.

Hadi kufikia jana, Marekani imerekodi waathiriwa milioni 2.3 wa virusi vya corona na zaidi ya vifo121, 000.

***BBC***




# KAKA:

## NEYMAR ANAWEZA KUSHINDA BALLON D'OR

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

NEYMAR ataongoza kwenye mbio za kuwania tuzo ya Ballon d'Or kama ataiwezesha Paris Saint-Germain kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya Agosti, mwaka huu, kwa mujibu wa Kaka.

PSG haijacheza mchezo wowote wa ushindani tangu Machi, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, ingawa walitawazwa kuwa mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, wakati msimu huu ulipofutwa Aprili.

Kikosi hicho cha Kocha, Thomas Tuchel kitakuwa fiti kuelekea kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kutokana na kuwa na zuio la safari za kimataifa kwa nchini za nchi nyingi za Ulaya, hatua ya nane bora itafanyika mjini Lisbon kwa mchezo mmoja tu na ndani ya siku 12, bingwa atakuwa ameshapatikana.

PSG itakuwa kwenye kinyang'anyiro hicho baada ya Neymar kufunga mabao kwenye mechi zote mbili hatua ya 16 na kuiondoa Borussia Dortmund kabla ya msimu kusimama.

Kaka alishinda Ballon d'Or mwaka 2007 na alikuwa mchezaji wa mwisho kishinda huku kukiwa hakuna jina la Cristiano Ronaldo au Lionel Messi hadi Luka Modric alipoitwaa mwaka 2018.

Nyota huyo wa zamani wa Real Madrid na Milan anafikiri PSG wanaweza kutwaa taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya na hilo litamfanya Neymar kuibeba tuzo hiyo.

Alipoulizwa kama kuna mchezaji yoyote kwa sasa wa Brazil anayeweza kutwaa Ballon d'Or, Kaka aliiambia Globo Esporte: "Wa kwanza ni Ney, ambaye ana nafasi kubwa ya kubeba.

"Naamini Neymar ni mmoja wa wachezaji bora wa leo. Kushinda tuzo hiyo kutategemea na mafanikio kwenye timu yake."

## CONTE ALALAMIKA MAMBO MAGUMU INTER



**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte amebainisha kushindwa kwa Inter Milan kubeba pointi zote tatu dhidi ya Sassuolo "kunamtesa", lakini kocha huyo anaamini kikosi chake kilistahili ushindi.

Bao la mapema la Francesco Caputo liliipa uongozi Sassuolo, lakini Romelu Lukaku na Cristiano Biraghi wakaiweka mbele Inter kabla ya mapumziko, kabla ya Roberto Gagliardini kukosa nafasi ya kufanya matokeo yawe 3-1.

Sassuolo walirudi mchezoni, bao la pili la Domenico Berardi dakika ya 81, kabla ya Borja Valero kufunga la tatu kwa Inter na Giangiacomo Magnani akasawazisha dakika za majeruhi.

"Nafikiri tulistahili ushindi, na hili limenichanganya," alisema Conte akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Ni kitu ambacho tunarudi mara kwa mara tunacheza vizuri, lakini hatupati matokeo. Inakatisha tamaa.

"Tulikuwa na nafasi nzuri ya kuibuka na ushindi katika mchezo huu, ili tujiweka kwenye nafasi nzuri ya mbio za ubingwa, lakini mambo yamekwenda tofauti kabisa."

## KOULIBALY NJIA NYEUPE KUTUA CITY

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City wana nafasi kubwa ya kumsajili, Kalidou Koulibaly kutoka Napoli, kwa mujibu wa mwandishi, Duncan Castles wa gazeti la Sunday Times.

Koulibaly ambaye ni mlinzi wa kati amekuwa akitajwa kuwaniwa na klabu kadhaa za Ulaya kwa muda mrefu sasa.

Lakini sasa inaonekana ana nafasi kubwa ya kujiunga katika Ligi Kuu England, wakati City wakitajwa kwamba wanafanyia kazi usajili huo.

Koulibaly kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na klabu za City, Liverpool, Manchester United, Tottenham, Real Madrid na Barcelona.

Lakini kwa mujibu wa Castles, Koulibaly sasa njia ni nyeupe kujiunga na kikosi cha kocha, Pep Guardiola kuliko kwa vinara wa ligi, Liverpool.

Inaelezwa kwamba usajili wake unaweza kufanyika kabla ya kuanza tena kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya Agosti 12.



HABARI MICHEZO



## MARTINEZ HAUZWI KOKOTE - MILAN

**MILAN, Italia**

OFISA Mtendaji wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, amesema klabu yake haina mpango wa kumuuza straika, Lautaro Martinez wakati huu akihusishwa na Barcelona.

Martinez amekuwa akitajwa zaidi kuwa mchezaji atakayeondoka Inter kwenda kwa mabingwa wa LaLiga, Barca mwisho mwa msimu huu 2019/20.

Barca imeripotiwa imekuwa kwenye wakati mgumu kufikia mahitaji ya Inter ambao wanakipengele cha kumuuza nyota huyo wa kimataifa wa Argentina kwa euro milioni 111.

Na sasa Marotta kwa mara nyingine alipoulizwa kuhusu Martinez baada ya mchezo wa sare ya 3-3 wa Jumatano dhidi ya Sassuolo, aliweka wazi kuwa hauzwi.

"Tumekuwa wazi kabisa kuhusu Lautaro, tukisema zaidi ya mara moja, Inter haina mpango wa kuuza wachezaji wake bora," alisema Marotta akiiambia DAZN.

"Suala la kuuzwa kwa Lautaro halipo na hatuna mpango huo, ni mmoja wa wachezaji wetu bora na tutaendelea kuwa nae."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 amefunga mabao 17 kwenye mashindano yote msimu huu kwa kikosi hicho cha Kocha, Antonio Conte.



## 'HAT-TRICK YA MARTIAL YAMKUNA MATIC

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa Manchester United, Nemanja Matic amemmwagia sifa mchezaji mwenzake, Anthony Martial baada ya kufunga hat-trick yake ya kwanza.

Martial alifunga mara tatu wakati United wakiifunga Sheffield United mabao 3-0 pale katika mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa juzi Jumatano kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Kipindi cha kwanza alifunga mabao mawili kabla ya kuongeza la tatu na kumfanya Martial kuwa mchezaji wa kwanza wa United kusherehekea 'hat-trick' kwenye Ligi Kuu tangu Robin van Persie alipofanya hivyo mwaka 2013.

Martial amefunga mabao 14 kwenye Ligi Kuu na 19 katika mashindano yote msimu huu na Matic amesifia fowadi huyo wa Ufaransa.

"Nafikiri ilikuwa ni muhimu kwake yeye kufunga mabao, kwa kila mshambuliaji ni muhimu," alisema Matic akiiambia MUTV.

"Nina furaha kwamba mshambuliaji wetu yupo kwenye hali nzuri, usiku ule Anthony alikuwa nyota wa mchezo, kila nafasi aliyoipata aliitumia vizuri.

"Ngoja tuangalie kwa siku za usoni nini atakachokifanya kwa upande wetu. Lakini nina furaha juu yake. Hongera sana kwake."

# NI HISIA NZURI LIVERPOOL KUBEBA EPL - SALAH

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah amesema huu ni wakati wa Liverpool kushinda taji la Ligi Kuu England baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Crystal Palace Jumatano.

Mabao kutoka kwa Trent Alexander-Arnold, Salah, Fabinho na Sadio Mane pale kwenye dimba la Anfield yalishuhudia kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kuendelea kujiweka pazuri zaidi kuelekea kutwaa ubingwa wake wa kwanza kwa kipindi cha miaka 30.

Liverpool kama jana Alhamisi Manchester City walishindwa kuifunga Chelsea pale Stamford Bridge basi itakuwa bingwa.

Na sasa Salah anasema huu ni wakati mzuri zaidi kwa Liverpool kutwaa ubingwa huo tangu mwaka 1990.

"Ni hisia nzuri kwa upande wetu sisi wachezaji," amesema akiiambia Sky Sports.

"Tangu nilipokuja hapa nilisema nataka kushinda taji la Ligi Kuu na timu hii. Na kwa sasa naona ndoto zetu zinakwenda kutimia.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ZIDANE AMPIGIA 'CHAPUO' RAMOS

Kocha huyo Mfaransa aeleza anaamini beki huyo mkongwe anastahili kustaafia soka kwenye kikosi cha Madrid...

**MADRID, Hispania**

KOCHA Zinedine Zidane, anaamini Sergio Ramos anastahili kustaafu soka akiwa na kikosi cha Real Madrid na anashangazwa kuona hatima ya mkataba wa beki huyo bado haieleweki.

Mkataba wa sasa wa Ramos kuitumikia klabu hiyo ya Bernabeu unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu wa 2020/21, muda ambao beki huyo wa kati atakuwa amefikisha umri wa miaka 35.

Uamuzi wa beki huyo kupewa mkataba mpya wa kuendelea kubakia klabuni hapo uko chini ya Rais wa Madrid, Florentino Perez.

Ramos hakuonyesha ishara yoyote ya kutaka kuondoka na amekuwa akiwashawishi wachezaji wenzake kujituma na kuchangia ushindi wa nne mfululizo wa mechi za LaLiga, ambapo Jumatano usiku waliichapa Real Mallorca mabao 2-0.

Ramos alifunga bao kwa mpira wa 'frikiki' na kuipa Real ushindi katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Alfredo di Stefano, na kumfanya beki huyo aweke rekodi ya kuwa mlinzi pekee aliyewahi kufunga zaidi ya mabao nane kwenye msimu mmoja wa LaLiga tangu Ezequiel Garay alipofanya hivyo msimu wa 2006/07.

"Sergio anastahili kubakia hapa kama mchezaji," Zidane aliwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo wa juzi.

"Amekuwa hapa kwa muda mrefu na anatakiwa kustaafu akiwa hapa. Hicho ndicho ninachokifiria na nitasimama nacho."

Ushindi huo wa Jumatano umeifanya Real kupanda kileleni mwa msimamo baada ya Barcelona kupoteza pointi kutokana na kulazimishwa sare ya bila kufungana na Sevilla katika mechi iliyochezwa Ijumaa iliyopita.

Mshambuliaji ambaye hayuko kwenye mipango ya mwalimu, Gareth Bale alianza katika kikosi cha kwanza cha Real ikiwa hajatapa nafasi hiyo tangu Februari, mwaka huu, lakini nyota huyo wa Wales alishindwa kuonyesha kiwango kizuri kwenye mchezo huo dhidi ya Mallorca iliyoko kwenye janga la kushuka daraja.

"Tuna furaha na namna tunavyoendelea kupambana na Gareth ni mmoja wa wachezaji muhimu, kila siku anathibitisha hilo," alisema Zidane.

## KWA UFUPI

**DYCHE KUITOSA BURNLEY**
KOCHA wa Burnley, Sean Dyche, ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu baada ya kutofurahishwa na hali ya kutotenga bajeti kwa ajili ya kuwaongezea mikataba na kusajili wachezaji wapya wa kuisaidia timu hiyo. ***(Mail)***

**KOULIBALY AKARIBIA CITY**
BEKI wa Napoli na Timu ya Taifa ya Senegal, Kalidou Koulibaly (29), anatarajia kujiunga na Manchester City ifikapo majira ya joto baada ya Liverpool kuamua kuachana na mchakato wa kumwania. ***(Express)***

**UNITED, SANCHO KITAELEWEKA**
MANCHESTER United ndio klabu pekee ambayo inawania saini ya winga wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (20), katika dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa. Lakini vigogo hao wa Bundesliga wanahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 118. ***(Bild - in German)***

**UNITED YAMBEBA FRED**
KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Brazil, Fred, ambaye ana umri wa miaka 27, anataka kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu ya Manchester United. ***(Sun)***

**WILLIAN KUPEWA MKATABA**
MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Willian (31), yuko katika mazungumzo ya kuongeza mkataba kabla ya kumalizika kwa msimu huu ili klabu hiyo kutoruhusu nyota huyo kuondoka akiwa mchezaji huru na kujiunga na mahasimu wao wa jiji la London. ***(Mail)***

**SILVA AKARIBIA ENGLAND**
EVERTON, Tottenham na Wolves zimeweka wazi nia ya kumsajili beki wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Brazil, Thiago Silva. Beki huyo mwenye umri wa miaka 35, anatajwa moyo wake sasa unataka kuona anasajiliwa na klabu yoyote ya nchini England. ***(Goal - in Portuguese)***

**ALCANTARA KUTUA LIVERPOOL**
LIVERPOOL imeonyesha nia ya kumsajili kiungo, Thiago Alcantara kwa dau la pauni milioni 43 baada ya mazungumzo ya kusaini mkataba mpya kati ya nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Hispania na klabu yake ya Bayern Munich kuvunjika. ***(Bild - in German)***

**ARSENAL, BARCA VITANI**
ARSENAL imeanza mawasiliano na Sporting Lisbon kwa ajili ya kuwania saini ya kinda mwenye kipaji Mreno, Joelson Fernandes (17). Mshambuliaji huyo chipukizi pia anawaniwa na Barcelona na RB Leipzig. ***(O Jogo via Star)***

**SALIBA KUBAKIA UFARANSA**
KOCHA wa Saint-Etienne, Claude Puel anataka kumpa mkataba mpya wa mkopo beki wa kati Mfaransa, William Saliba (21), ambaye alijiunga na timu hiyo akitokea Arsenal baada ya kumalizika kwa mechi ya fainali ya Kombe la Ufaransa. ***(Goal)***

**NDOMBELE AMKATAA MOURINHO**
NYOTA aliyeweka rekodi ya usajili katika kikosi cha Tottenham kwa kusajiliwa kwa dau la pauni milioni 54, Tanguy Ndombele (23), amemweleza Kocha, Jose Mourinho kuwa hataki tena kucheza chini yake. Paris St-Germain, Barcelona na Bayern Munich zinamwania kiungo huyo wa Ufaransa. ***(ESPN)***

**MOUNT AFANYA KWELI**
KIUNGO wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Mason Mount (21), amewanunulia tiketi za kuingia uwanjani wafanyakazi wa afya za kuiona timu ya Vitesse Arnhem ya Uholanzi, baada ya kuitumikia kwa mkopo klabu hiyo katika msimu wa 2017/18. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# NAMUNGO YAWEKA REKODI, 'YATINGISHA' LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

SARE ya mabao 2-2 iliyopata Namungo FC dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jumatano iliyopita, imefanya timu hiyo kucheza mechi 15 mfululizo za Ligi Kuu Bara bila kupoteza, ikiwa katika nafasi ya nne na pointi zake 55.

Namungo imeweka rekodi ya msimu, kwani hakuna timu yoyote kwenye Ligi Kuu ambayo imecheza idadi hiyo ya mechi bila kupoteza.

Simba inafuatiwa kwa kucheza mechi 12 mfululizo bila kupoteza, huku Yanga ikishika nafasi ya tatu kwa kuweka kucheza mechi 11 bila kupoteza msimu huu.

Kwa sasa hakuna timu itakayoweza kuweka tena rekodi hiyo, kwani kama Simba isipopoteza mechi yoyote itakuwa imecheza mechi 11 bila kupoteza na Yanga itakuwa imecheza mechi 12, kwa michezo yao ambayo imebakisha.

Mara ya mwisho kwa Namungo kupoteza mechi ilikuwa ni Januari 29, mwaka huu, ilipochapwa mabao 3-2 dhidi ya Simba na baada ya hapo imecheza mechi 15 bila kupoteza, ikishinda mechi tano na kutoa sare 10.

Namungo ilianza kuonyesha makali yake kwa kuinyuka Mbao FC mabao 3-0, kabla ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Alliance FC halagu ikatoka sare ya bila kufungana dhidi ya Ndanda, kabla ya kuichapa Singida United bao 1-0, baadaye ikalazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mwadui FC.

Ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya KMC, na kuichapa Azam bao 1-0, pia ikaisasambua Lipuli mabao 2-1.

Baada ya hapo ikaanza kutoa sare mfululizo ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar, bila kufungana dhidi ya Polisi Tanzania, sare ya bao 1-1 dhidi ya Biashara United na pia sare kama hiyo dhidi ya Yanga hiyo ikiwa ni mechi ya mzunguko wa kwanza na iliporejea baada ya mapumziko ya janga la corona ilianza kwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Coastal Union na kuichapa Kagera Sugar mabao 2-0.



Wachezaji wa Yanga Princess wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Karume jijini, Dar es Salaam ili kujiandaa na mechi za Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania inayotarajiwa kurejea tena kuanzia keshokutwa. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Nahodha Mwadui apata 'ulaji'

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Mwadui FC, Joram Mgeveke, anatarajia kujiunga na Chipa United inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza nchini Afrika Kusini, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Wakala wa mchezaji huyo, George Peter, alisema mazungumzo ya kujiunga na timu hiyo yanakwenda vizuri na wanatarajia kumpa mkataba wa miaka miwili.

Peter alisema timu hiyo imekuwa ikimfuatilia nyota huyo kwa muda mrefu kwa kuangalia video mbalimbali za michezo anayocheza na sasa wameanza taratibu za kumsajili.

"Ni kweli Chipa United inamhitaji Joram, endapo makubaliano yataenda sawa ataenda kuichezea, lengo ni kutaka afike mbali zaidi aweze kutimiza malengo yake ya kusajiliwa Ulaya, "alisema wakala huyo.

Peter alisema Uongozi umeahidi kumuongezea mkataba kama wataridhishwa na kiwango atakachokionyesha katika kikosi hicho.

"Mipango ikikamilika, tutaweka wazi kila kitu ili Watanzania wafahamu kinachoendelea kuhusu mchezaji huyo, tunaamini mambo yatakamilika na ndoto zake kuanza kutimia," wakala huyo alisema.

Naye Mgeveke alisema lengo lake ni kucheza soka la kulipwa ili atimize malengo ambayo amekuwa nayo kwa muda mrefu na kuwaomba Watanzania wazidi kumwombea dua.

Mgeveke alisema anatamani kufika mbali zaidi kwa kutumia vema kipaji chake kama alivyofikia nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) na Aston Villa, Mbwana Samatta.

## Serikali yarejesha Ligi Kuu Pemba

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

HATIMAYE Ligi Kuu Zanzibar ambayo inatarajiwa kurejea tena kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, sasa itachezwa katika vituo viwili vya Unguja na Pemba, imeelezwa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitangaza ligi hiyo itachezwa katika kituo kimoja cha Unguja ikiwa njia moja ya kukabiliana na virusi vya ugonjwa wa corona.

Kaimu Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Vuai Ame, alisema serikali imeridhia ligi hiyo kuchezwa katika vituo viwili badala ya kituo kimoja kama ilivyotolewa hapo awali lakini itachezwa bila ya mashabiki.

Ame alisema wahusika wa ligi hiyo watatakiwa kuchukua tahadhari zote za kujikinga na corona kama zilivyotolewa na wataalmu wa afya.

"ZFF imevitaka vilabu vyote vya Ligi Kuu kuendelea kuchukua tahadhari zote za kujikinga na corona katika sehemu wanazofanyia mazoezi," Ame alisema.

Julai Mosi, mwaka huu kutakuwa na michezo minne ambapo Selem View itawakaribisha Mafunzo kwenye Uwanja wa Gombani huku Jamhuri ikiwavaa Polisi wakati Zimamoto itawakabili Mlandege na JKU watapepetana na Maafande wenzao wa Kipanga.

## Ndanda yaipigia mahesabu Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Ndanda FC, Abdul Mingange, ameweka wazi sasa anahitaji kukusanya pointi nane katika michezo yao yote iliyobakia ukiwamo dhidi ya Yanga utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili Mingange, alisema bado yupo katika hali mbaya ya kujinusuru na janga la kushuka daraja hivyo wanapambana kutafuta pointi katika kila mechi watakayocheza.

Mingange alisema anahitaji kumaliza ligi akiwa na alama 43, hivyo analazimika kufanya vizuri katika kila mechi watakayocheza ili kubakia tena kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 msimu huu.

"Nahitaji pointi kutoka kila mechi, haijalishi nakutana na timu gani, nimeshuhudia Yanga katika michezo miwili, ikiwamo walipocheza dhidi ya Azam, tayari nimeanza kufanyia kazi upungufu na ubora wa Yanga," alisema Mingange.

Aliongeza mipango yake ni kujiondoa kwenye hatari ya kushuka daraja kabla ya mechi ya mwisho na anawaambia mashabiki wa Ndanda wasiwe na wasiwasi.

"Ndanda haiwezi kushuka daraja, nimeweka mipango sawa na nimeongea na wachezaji wangu, wamenihakikishia kupambana kutafuta alama muhimu katika kila mchezo," alisema Mingange.

Michezo
Ijumaa Juni 26, 2020
Nipashe



## Zidane ampigia 'chapuo' Ramos

HABARI UK 22



Kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa Sheffield United, Jack Robinson katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. United ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAPATA 'PIGO' LINGINE

●●●Beki wake kisiki afungiwa mechi tatu, huku kocha Mbelgiji akilalamika washambuliaji kumwangusha...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, akiwatupia lawama washambuliaji wake kwa kushindwa kutumia nafasi walizozitengeneza katika mchezo dhidi ya Namungo uliomalizika kwa sare ya mabao 2-2, beki wake wa kati, Lamine Moro amefungiwa kucheza michezo mitatu.

Adhabu hiyo imekuja siku chache baada ya winga wao, Bernard Morrison kufungiwa mechi mbili pamoja na kutozwa faini ya Sh. 500,000 kutokana na kufanya vitendo visivyokuwa vya kiungwana.

Lamine pia amepigwa faini ya Sh. 500,000 na Bodi ya Ligi.

Eymael aliliambia gazeti hili baada ya mchezo huo kumalizika kuwa washambuliaji wake ndio walioinyima timu hiyo ushindi kwa sababu ya kutokuwa makini kwa kupoteza nafasi nyingi hasa dakika 45 za kipindi cha kwanza.

Mbelgiji huyo alisema washambuliaji wake wangekuwa makini na kutumia vema nafasi walizopata, ana imani wangeenda mapumziko wakiwa mbele kwa mabao 3-1.

"Nimefanya kazi yangu ipasavyo, ila bado kazi kubwa ipo kwa washambuliaji, kukosa nafasi nyingi za wazi kwa kutokuwa makini," alisema Eymael.

Kocha huyo alisema hajafurahishwa na matokeo hayo ambayo yanawaweka kwenye wakati mgumu wa kumaliza msimu katika nafasi ya pili ambayo inawaniwa pia na timu nyingine ikiwamo Azam FC.

"Wachezaji wamepambana ila kuna jambo linalishangaza, na hili lipo hapa Tanzania kwa uamuzi unaofanywa na waamuzi," Eymael alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania, Almasi Kasongo, alisema katika taarifa yake Lamine amefungiwa mechi tatu na kupigwa faini ya Sh. 500,000 kwa kosa la kumkanyaga mchezaji wa JKT Tanzania, Mwinyi Kazimoto katika mechi iliyochezwa Juni 17, mwaka huu jijini Dodoma.

> **"Kamati imeiomba Yanga kukaa na mchezaji wao huyo (Lamine), kumkumbusha kuhusiana na mchezo wa kiungwana anapokuwa kwenye majukumu ya kuitumikia klabu hiyo," Kasongo alisema.**

Aliongeza Bodi ya Ligi imepeleka malalamiko ya Azam FC kuhusu uamuzi uliofanywa katika mchezo wao dhidi ya Yanga katika Kamati ya Waamuzi.

"Katika malalamiko yao, Azam wamedai walipaswa kupewa mabao mawili na penalti moja baada ya mchezaji wao kuangushwa ndani ya eneo la penalti," alisema kiongozi huyo.

Alisema pia JKT Mlale ya Songea, imepoteza mchezo wake wa Ligi Daraja la Kwanza dhidi ya Dodoma FC, kwa sababu mashabiki wake walivamia uwanjani na kumshambulia mwamuzi wa kati na mwamuzi msaidizi namba mbili na kusababisha mchezo huo kuvunjika.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 43 (4), ya Ligi Daraja la Kwanza, Dodoma FC inapewa ushindi wa pointi tatu na mabao matatu, huku Mlale ikitozwa faini ya Sh. 500,000 wakati Kocha Msaidizi wa Maafande hao, Rashid Mpenda, akitozwa faini ya Sh. 300,000 na kufungiwa miezi sita kwa kosa la kushambulia waamuzi.

## USHINDANI BARA WAKOLEA MKIANI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikielekea ukingoni, vita ya juu ya kuwania ubingwa inaonekana imemalizika, baada ya Simba kuhitaji pointi mbili tu ili itwae ubingwa, sasa vita hiyo inaonekana kuhamia chini kwa timu zinazotaka kujiepusha kushuka daraja.

Jumla ya timu tisa zinaonekana ziko kwenye hali tete, ambapo zitatakiwa kupambana kwa hali na mali kuhakikisha zinashinda ili kujiweka kwenye sehemu salama.

Timu hizo ni Singida United inayoshika mkia, Mbao FC, Mbeya City, Alliance FC, Lipuli FC, Ndanda FC, Mwadui FC na Mtibwa Sugar.

Msimu huu, timu nne kuanzia itakayoshika nafasi ya 17 hadi ya 20, zitashuka daraja moja kwa moja, huku zitakazoshika nafasi ya 15 na 16 zitapata nafasi ya kucheza mechi za mtoano na timu zitakazoshika nafasi ya pili kwenye Ligi Daraja la Kwanza.

Singida United ni kama vile inasubiri siku ya kutangazwa rasmi kushuka, kwani baada ya kuchapwa mabao 3-1 nyumbani dhidi ya Mtibwa Sugar, imebakiwa na pointi zake 15 tu, ikizidiwa pointi 11 na timu ya Mbao FC iliyo juu yake.

Endapo Singida United itashinda zote zilizobakia, itafikisha pointi 36 ambazo tayari timu ya KMC ya Kinondoni inazo wakati Mbao FC nayo, pamoja na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union, bado haikuifanya timu hiyo kusogea hata nafasi moja, badala yake imebaki pale pale kwenye nafasi ya 19, ikiwa imefikisha pointi 26.

Baada ya kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Simba, Mbeya City imebakiwa na pointi 30, ikiwa kwenye nafasi ya 18, nayo itakuwa na kazi ya ziada katika mechi zake saba zilizobaki huku Alliance FC iliyolazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania, mpaka sasa inamiliki pointi 33, ikiwa kwenye nafasi ya 17, nayo haiko kwenye nafasi salama.

Hali ya kushangaza inaonekana kwa Lipuli FC ambayo msimu uliopita ilikuwa 'moto' lakini msimu huu makali yake yamepungua na kutakiwa kujinasua na hatari ya kushuka daraja wakati Ndanda yenye pointi 35, nayo haiko kwenye nafasi nzuri, ingawa misimu yote ni timu yenye bahati ya kuepuka kushuka daraja kwenye mechi za mwisho.

Baada ya kuchapwa mabao 4-0 dhidi ya Biashara United, KMC nayo imerudi kule kule katika nafasi hatari sawa na Mwadui FC ambayo pointi 37 na katika msimamo iko kwenye nafasi ya 13.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >